SportPesa
TZS. 517,350,800
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**CHADEMA** yafanya utafiti kubaini kiini tatizo la machinga

UKURASA 3


Watanzania tatizo si utawala bora, shida kubwa ni uchumi
siasa
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe
VLADIMIR PUTIN
Miongo miwili madarakani, ataishi ikulu hadi 2036
Ziara ya Chongolo, timu yake inavyowabana mubashara viongozi wanaolalamikiwa
•Yaanza na Byabato vipi kukatika umeme ovyo
•Shaka amvaa waziri kwa simu 'live' kieleweke

UKURASA 11

# Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatano Septemba 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580711
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Askofu akemea wanaopewa vyeo kwa kujipendekeza



Askofu Benson Bagonza.

**•Agusia** Katiba Mpya, Ulimwengu aguna ubora wa elimu... *Endelea ukurasa 2 & 3*




Familia ikitoa heshima za mwisho kwa mwili wa Prof. Matthew Luhanga, wakati wa ibada ya kumuaga katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Andrea Mtume, Bahari Beach, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Familia yapoteza ndugu saba ndani ya siku 10

UKURASA 2

UKURASA WA 4

### VYAMA VYALIA WAGOMBEA WAKE UDIWANI KUENGULIWA

SIKU moja baada ya wagombea 10 wa vyama vya upinzani, kuenguliwa kuwania udiwani katika uchaguzi wa Kata ya Ndembezi Manispaa Shinyanga, viongozi wa vyama vya siasa wamesema ni kupuuzwa kwa kauli ya Rais Samia Hassan.

Agosti 21, mwaka huu, Rais Samia, akipokea...

UKURASA WA 4

### CHADEMA YADAI POLISI KUZINGIRA OFISI KIKAO NDANI

ZAIDI ya askari 10 baadhi yao wakiwa na silaha za moto wamedaiwa kuzingira ofisi za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Mbeya, katika kikao cha ndani cha viongozi wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA)...



UKURASA WA 8

### MBARAWA ATAKA DARAJA WAMI KUJENGWA SAA 24

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amemwagiza mkandarasi anayejenga daraja la Wami kufanya kazi saa 24 ili kukamilisha kazi kwa wakati...

### Dk. Shein aongoza maziko ya Prof. Luhanga

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YAPEWA MBINU KUIUA MAPEMA JWANENG GALAXY UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akikagua tangi la maji katika Mradi wa Maji wa Kemondo, wilayani Kigoma, jana. Wapili kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali, Charles Mbuge. **PICHA: OWM**

# Askofu akemea wanaopewa vyeo kwa kujipendekeza

**Na Richard Makore, MWANZA**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Dayosisi ya Karagwe mkoani Kagera, Benson Bagonza, amekemea tabia ya kusifia viongozi waliopo madarakani, akishauri iwe miongoni mwa makosa ya jinai nchini, ili kupunguza watu kujipendekeza kwa lengo la kupata vyeo.

Akizungumza jana jijini Mwanza wakati wa uzinduzi wa kitabu cha mwandishi mkongwe nchini, Jenerali Ulimwengu, Askofu Bagonza alisema, watu wengi wanashindwa kufanya kazi walizokabidhiwa kuzifanya badala yake wanaweka nguvu kusifia viongozi.

**"Watanzania wanahitaji katiba yenye uwezo wa kuweka na kuwaondoa viongozi madarakani badala ilivyo kwa sasa," Askofu Bagonza alisema.**

Alisema baadhi ya viongozi wa serikali ngazi za chini wamekuwa na tabia hiyo na kumtwisha Rais mzigo ambao hastahili kutwishwa.

Askofu Bagonza alisema kielelezo kizuri ni Hayati Benjamini Mkapa aliyewahi kutamka bayana kwamba lugha nzuri ya kutumia ni kuiita serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) badala ya nadharia iliyotaka kujengwa ya Serikali ya Magufuli.

Alikumbusha kuwa Hayati Mkapa alitoa angalizo hilo mbele ya Hayati Dk. John Magufuli alipowaita na kufanya mazungumzo na viongozi wastaafu Ikulu jijini Dar es Salaam.

"Kama ni kiongozi wa chini afanye kazi yake na siyo kubakia anasifia tu Rais, yaani hata choo kikijengwa, anasema Rais ameleta hela ya kujenga choo hiki," alisema Askofu Bagonza.

Alifafanua kuwa imekuwa kawaida hata kwenye misiba mtu anasimama anasema anampongeza Rais, jambo ambalo ni baya kwa kuwa kiongozi huyo anatwishwa mizigo isiyomhusu.

Kiongozi huyo wa kiroho alifafanua kuwa ubaya wa kumsifia Rais kila mahali ni pamoja na kumfanya aone wasiomsifia katika jamii labda hawampendi, jambo ambalo siyo sahihi.

Askofu Bagonza alisema hali hiyo inawafanya viongozi wasiofanya kazi zao vizuri, waishie kumtaja na kumsifia Rais ili ionekane wamefanya kazi zao vizuri.

Pia alikemea kitendo cha viongozi kusema fedha zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo, zimetolewa na Rais, akionya kuwa kufanya hivyo kunasababisha baadhi ya wananchi washindwe kulipa kodi za serikali wakiamini kwamba kiongozi huyo ana fedha nyingi.

Akizungumzia uchaguzi na haki za binadamu nchini, Askofu Bagonza alisema ili uwe kiongozi mzuri ni lazima jamii iliyokutuma ikuchague kwa kura zao na kwa njia halali kwa mujibu wa katiba za vyama na Katiba ya nchi.

Akizungumzia umuhimu wa kuwa na Katiba Mpya, Askofu Bagonza alisema Hayati Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema marais wazuri wanatakiwa kuongoza kwa vipindi viwili ili waondoke na uzuri wao, lakini marais wabaya wataondolewa na wananchi.

Alisema katiba nzuri ni silaha kubwa kwa wananchi kwa sababu wanaweza kuitumia kuweka madarakani viongozi wazuri na kuwaondoa katika uongozi wale wabaya muda wowote watakapotaka.

"Watanzania wanahitaji katiba yenye uwezo wa kuweka na kuwaondoa viongozi madarakani badala ilivyo kwa sasa," Askofu Bagonza alisema.

**KATIBA MPYA**

Katika uzinduzi wa kitabu hicho, Ulimwengu alisema amelazimika kuandika kitabu hicho ambacho kimebeba makala zake zote tangu mwaka 1996 kwa kuwa anaamini mawazo yake mpaka sasa hayajabadilika.

Alisema makala zake hata kama aliziandika zikiwa za kijiunga kwa wakati huo, lakini bado anaamini mawazo na fikra zake za wakati huo bado hazijabadilika mpaka sasa.

Kuhusu Katiba Mpya, aliwataka Watanzania kuanza kuchambua vipengele ambavyo wangependa viwamo katika Katiba Mpya hiyo ili wakipata wasaa wavijadili badala ya kusema tu wanataka Katiba Mpya kwa ujumla wake.

**UBORA WA ELIMU**

Akizungumzia suala la mfumo wa elimu nchini, Ulimwengu alisema bado una matatizo mengi na kwamba haumwandai mtu kutengeneza kitu cha kulisaidia taifa.

"Hakuna uwezekano wa kizazi chetu kupata maendeleo na kupiga hatua ikiwa kitaendelelea kufundishwa kwa lugha wasioijua na pia wale wanaowafundisha nao hawaijui hiyo lugha," Ulimwengu.

Katika uzinduzi huo, Ulimwengu alitia saini na kukiuza kitabu chake hicho kwa baadhi ya washiriki wakiwamo waandishi wa habari pamoja na wanaharakati kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Kitabu hicho kimepewa jina la 'Rai ya Jenerali Ulimwengu', kikiandikwa na mwandishi nguli huyo.

# Familia yapoteza ndugu saba ndani ya siku 10

**Na Mwandishi Wetu**

WATU saba wa familia moja wamepoteza maisha kwa kipindi cha siku 10, wakiwamo watano waliofariki dunia jana kwenye ajali ya gari iliyohusisha gari ndogo na lori wakitokea mkoani Mbeya walikokwenda kuhudhuria maziko ya ndugu yao.

Tukio hilo lilitokea jana eneo la Inyala mkoani Mbeya, watu watano wakifariki dunia, akiwamo mtoto.

Mmoja wa wanafamilia, Bupe Mboya, aliiambia Nipashe jana kuwa alipata taarifa ya ajali hiyo jana asubuhi ikiwa ni wiki moja tangu aliporejea kutoka mkoani Mbeya kwa mazishi ya mmoja wa wanafamilia.

"Baada ya kuzika Mbeya, ndugu yetu ambaye alifariki dunia Dar es Salaam na kusafirisha, imepita wiki moja, tulio wengi tulirudi na Costa kuja Dar baada ya maziko.

"Tukamwacha Tom (marehemu) na ndugu wengine wakisema watafuata siku chache baadaye kwa gari ndogo.

"Waliofariki dunia wote ni familia moja. Hapa nipo na mke wa marehemu kwa ajili ya kupanga safari ya kurudi tena Mbeya kwa mzishi kwa sababu miili ya marehemu imehifadhiwa Mbeya," alisema Bupe.

Alibainisha Septemba 13, mwaka huu, yaani siku tisa zilizopita, familia hiyo ilipoteza mmoja wa wanafamilia na kuzikwa mkoani Dar es Salaam.

Aliendelea kusimulia kuwa Septema 15, mwaka huu, alifariki dunia mwanafamilia mwingine na kwamba wawili hao walikuwa wagonjwa hadi umauti unawafika.

"Siku 10 yaani haizidi wiki moja alifariki ndugu yetu na tulizika Kurasini. Baada ya siku tatu, tarehe 15 akafariki dada wa huyu tuliyemzika Kurasini.

"Huyu dada ndiye tulimsafirisha kwa ajili ya maziko na wakati wanafamilia tukirudi Dar es Salaam, ndugu zetu wakapata ajali na kufariki watano leo (jana)," alisema.

Kwa mujibu wa Bupe, ndugu waliofariki dunia jana kutokana na ajali hiyo ni: Thomas Mboya; Isabela Mboya; Joyce Mboya; Magreth Masaka; na Seviline Mgalla.

Jana mchana, Nipashe ilipowasiliana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alidai hakuwa na taarifa za ajali hiyo inayodaiwa kusababisha vifo vya ndugu hao.

Hata hivyo, majira ya saa 12 jioni, kiongozi huyo wa polisi alibainisha kuwa jeshi hilo lilikuwa linaandaa taarifa rasmi kuhusu tukio hilo.

## HABARI KITAIFA




Wafanyabiashara wakiendelea na shughuli zao licha ya kuwapo bango la amri ya kutofanya biashara kwenye eneo hilo, lililowekwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), katika Barabara ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CHADEMA yafanya utafiti kiini tatizo la machinga

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema kitafanya utafiti kuhusu wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, kufanya biashara katika maeneo yasiyokuwa rasmi ili kupata njia sahihi za kutatua vikwazo vilivyoibuka.

Akizungumza na Nipashe mkoani Dar es Salaam jana, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Benson Kigaila, alisema hawakubaliani na kile kinachofanywa na serikali kwa sasa na kusema ipo haja ya kulifanyia utafiti wa kina suala hilo kabla ya kutoa uamuzi.

"Suala la machinga ni kubwa sana, sisi tunalifanyia utafiti serious (makini), tunajua impact (athari) yake ni kubwa sana, tunajua kila mwaka nchi hii inazalisha vijana kutoka vyuo mbalimbali ambao hawana ajira.

"Tunajua nchi hii haizalishi ajira yoyote, nchi hii imekaa kiuchuuzi na ndiyo maana tunaongea habari ya machinga, maana yake machinga ni watu wanaouza vitu, huyu akimaliza atataka auze vitu na yule auze vitu sasa tutamuuzia nani?

"Sisi tutalifanyia utafiti mpana ili tukilisemea hili suala kama msimamo wa chama ambao ni mpana uwe na majibu, hawa jamaa hawana jibu la hiyo kitu, sisi tunataka tutengeneze utafiti wa kutosha tujue shida, ukubwa wake na inaweza kukabiliwa namna gani," alisema.

Hivi karibuni Mbunge wa Kuteuliwa, Humphrey Polepole, aliyewahi kuwa Katibu Mwenezi wa CCM, alisema ni vyema kuzingatia uchambuzi wa wadau kuhusu uhakika wa kupata soko kwa bidhaa za machinga katika maeneo ambapo serikali imepanga kuwahamishia ili kutokuwarudisha nyuma kiuchumi.

Wiki iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan, akiwaapisha mawaziri Ikulu mkoani Dodoma, aliagiza wakuu wa wilaya na mikoa nchini kuwapanga vyema na kuonya anayoyaona kwenye runinga ya ngumi, kupigana, kufukuzana, kuchafuliana na vitu kumwagwa kwamba sasa hataki kuyaona tena.

Tayari katika maeneo kadhaa nchini ikiwamo katika majiji ya Dar es Salaam na Mwanza tahadhari imeshatolewa kwa machinga ikiwamo kuweka mabango kuwazuia kufanya biashara katika mifereji ya maji, njia za wapita kwa miguu, hifadhi za barabara na mbele ya maeneo ya taasisi za umma kama shuleni.

***Imeandaliwa na Enock Charles, Leyla Joho (TUDARCo) na Polin Lugaziya (SJMC).**

## Dk. Shein aongoza maziko ya Prof. Luhanga

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Chuo cha Mzumbe, Dk. Mohamed Ali Shein ameongoza waombolezaji katika maziko ya aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Matthew Luhanga, aliyezikwa kwenye makaburi ya Kwa Kondo, Tegeta jana jijini humo.

Prof. Luhanga alifariki dunia Jumatano iliyopita na maziko yake yalitanguliwa na ibada ya mazishi iliyofanyika Parokia ya Mt. Andrea Mtume, Bahari Beach.

Viongozi wengine waliohudhuria ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, baadhi ya wakuu wastaafu wa chuo cha Mzumbe, UDSM na wasomi mbalimbali waliowahi kufanya naye kazi.

Katekista Robert Ikombe, alisema Prof. Luhanga alikuwa muumini wa kanisa hilo na alikuwa mwenye upendo na kujali.

"Nimebahatika kuongea naye mara nyingi, ulikuwa ukikaa naye hajivunii kwamba yeye ni msomi kwamba hawezi kuongea na mtu mwingine yeyote, alikuwa mtu anayepokea ushauri unaompa, alikuwa mtu wa watu," alisema.

Katekista Ikombe aliwaasa waumini kuwa maisha ni mafupi na kuwataka wafanye kazi ya Mungu kwa kuishi anavyoelekeza kuwapenda na kuwatumikia wale ambao wamekabidhiwa.

"Prof. Luhanga alikuwa na mamlaka makubwa, lakini katika maisha yake bado aliweza kutumika kwa hali yoyote ile," alisema.

Mercy Luhanga, alisema Prof. Luhanga ni baba yake mdogo na alimlea, alikuwa kiongozi anayejali muda na mchapa kazi ambaye pamoja na majukumu mbalimbali alikuwa anajali familia.

"Wengi walipenda kumuita mbishi, alipenda kusimamia jambo ambalo aliliamini liko sawa," alisema.

Prof. Anagisye alisema yapo mengi ya kujifunza kutoka kwa Prof. Luhanga ambaye akiwa Makamu Mkuu wa Chuo cha UDSM alibeba mzigo kwa ajili ya maendeleo ya chuo, kiongozi, mtafiti, mwanataaluma na mwadilifu na mzalendo ambaye aligusa maisha ya Watanzania na wataaluma wengine duniani.

Alisema Prof. Luhanga alikuwa jabali la mageuzi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya taaluma, utafiti, miundombinu na chuo kwa ujumla pia, sehemu ya msingi alioanzisha kwenye chuo hicho.

Mhadhiri Mwandamizi Masuala ya Mipango ya Elimu, Prof. Herme Mosha, alisema Prof. Luhanga alikuwa mtu wa kuthubutu hata itoke amri kutoka serikalini alikuwa haikubali hivi hivi bila kutafakari.

"Alikuwa mtu anayeweka muda, aliheshimu watu na kila mtu alimuheshimu, vijana wajifunze kupitia yeye," alisema.

Prof. Luhanga aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu Mzumbe.

## PM avihakikishia vijiji vyote majisafi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameweka mikakati madhubuti inayolenga kumaliza tatizo la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika vijiji vyote nchini vikiwamo vya wilaya ya Bukoba mkoni Kagera.

Amesema serikali inaendelea kutekeleza kampeni ya Rais Samia ya kumtua mama ndoo kichwani ili kuhakikisha huduma hiyo inapatikana karibu na kuwawezesha wanawake na vijana katika maeneo mbalimbali nchini hususani ya vijijini kupata muda wa kushiriki katika shughuli za kijamii.

Majaliwa ametoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wananchi katika Kata ya Kemondo baada ya kukagua ujenzi wa mradi wa maji wa Kemondo-Maruku akiwa katika katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mkoa huo.

Waziri Mkuu alisema serikali imeweka mikakati madhubuti yenye lengo la kumaliza tatizo la maji nchini, hivyo wananchi waendelee kuwa na subira kwani mradi huo utakamilika kwa wakati na kwa viwango ili wapate huduma hiyo kama ilivyokusudiwa.

Awali, Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Mazingira Vijijini (RUWASA) wilaya ya Bukoba, Mhandisi Evaristo Mgaya, alisema mradi huo unalenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika kata tano za wilaya ya Bukoba na moja ya Wilaya ya Muleba.

Mhandisi Mgaya alisema mradi huo unaotekelezwa kwa awamu, ya kwanza itahusisha kata mbili za Kemondo na Maruku kwa gharama ya Sh. bilioni 6.8, ambapo alitaja baadhi ya kazi zinazoendelea kuwa ni pamoja na ujenzi wa tanki la lita milioni tatu, uchimbaji wa mitalo ya kulazia mabomba ya kusambazia maji.

"Mradi huu umelenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika vijiji vya kata za Kemondo, Maruku, Kanyangereko, Bujugo na Katerero wilayani Bukoba na Kata ya Muhutwe wilayani Muleba. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu na umekadiriwa kunufaisha wananchi 117,461 kwa gharama ya Sh.bilioni 15.9."

Baada ya kukagua ujenzi wa mradi wa maji, Waziri Mkuu alikagua mradi mwingine wa ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Bukoba inayojengwa katika kata ya Bujunangoma, ambapo aliwaagiza viongozi wa Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Bukoba wahakikishe wanasimamia kwa karibu miradi hiyo.

*The Following USED Machine are available for immediate sales.*

Motor Grader







116470902

Managing Director
Estim Construction Co. Ltd, P.O. Box 19716
For Further Enquiry, please contact. 0784261345, 0746941956

# Vyama vyalia wagombea wake udiwani kuenguliwa

**Mary Geofrey na Marco Maduhu**

SIKU moja baada ya wagombea 10 wa vyama vya upinzani, kuenguliwa kuwania udiwani katika uchaguzi wa Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, viongozi wa vyama vya siasa wamesema ni kupuuzwa kwa kauli ya Rais Samia Hassan.

Agosti 21, mwaka huu, Rais Samia, akipokea Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, alisema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutokata majina ya wagombea walioshindwa kujaza fomu za kuwania na badala yake warekebishe makosa na kuendelea na taratibu.

"Suala hili kwa sasa litaangaliwa vizuri lakini muwe makini vinginevyo... ushauri uliotolewa hapa utatiliwa maanani na yale yote yatakayokwenda kuchambuliwa baada ya ripoti hii, serikali itayachukua na kuyafanyia kazi ipasavyo," alinukuliwa Rais Samia.

Mwenyekiti wa Chama cha UPDP Taifa, Twalib Kadege, alisema NEC wanakiuka agizo la Rais Samia la kuwataka kutowafutia wagombea kuwania nafasi kwa sababu ya kukosea kujaza fomu na makosa mengine madogo.

Alisema siyo mara ya kwanza kutokea kwa vyama vya upinzani wagombea wao kuenguliwa, hivyo vyama vilivyokutana na adha hiyo vinapaswa kukata rufani.

"Wengine inawezekana ni kweli wameshindwa kukidhi vigezo na wengine unawezakuta wamekatwa kwa makusudi hivyo ni suala la kufuatilia na kuweka pingamizi ili wanaokidhi vigezo warudishwe," alisema Kadege.

Alisema tatizo la vyama vya siasa kutokuwa makini katika kufuata vigezo ni sababu za kuenguliwa katika chaguzi nyingi zinazofanyika nchini.

Alisema kuna umuhimu wa vyama vya upinzani kukaa na NEC kuangalia makosa kama hayo yarekebishwe na warudishwe wawanie uchaguzi.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha CHAUMA, Hashimu Rungwe, alidai ni hujuma zinazofanywa na vijana wa usalama wa Taifa ambao wanawarubuni wagombea kwa fedha ili wasiwania nafasi hiyo na mgombea wa CCM aibuke mshindi.

"Ni hujuma tu zinazoendelea na siyo kweli kuwa wagombea wote wamekosea kujaza fomu au masharti ya kuwania nafasi hii," alidai Rungwe.

Alisema suluhisho la changamoto hiyo ni kupatikana kwa Katiba Mpya vinginevyo mambo hayo yataendelea kuwapo katika chaguzi zote.

Naye Naibu Katibu wa Uenezi na Uhusiano kwa Umma wa Chama cha ACT-Wazalendo, Janeth Rithe, alisema wanasheria wao wanashughulikia suala hilo.

Alisema wanaangalia ni makosa yapi yaliyofanywa mgombea wa chama chao aenguliwe kuwania nafasi hiyo ili wakate rufani.

Naye Mgombea Urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Chama cha NRA, Mahona Leapald, aliwalaumu viongozi wa vyama vya siasa kusimamia maslahi binafsi badala ya wananchi.

Alisema suala hilo limetawaliwa na rushwa kwa sababu katika hali ya kawaida haiwezekani wagombea wote 10 kushindwa kukidhi vigezo vya kuwania nafasi hiyo.

Alisema wananchi wanapaswa kuamua kama kufuta vyama vya upinzani na kuendelea kukiishi CCM pekee vinginevyo siasa hazina maana.

Juzi Msimamizi wa Uchaguzi huo mdogo wa kata ya Ndembezi, Timothy Andrew, aliweleza waandishi wa habari kuwa, baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzani hawakukidhi vigezo vya kuwania udiwani huku wengine wakishindwa kurudisha fomu kwa wakati.

Aliwataja wagombea walioenguliwa kuwa ni Abdalla Sube wa Chama cha Demokrasia Makini, Rehema Mjengi (ACD), Antony Ndinda (SAU), Ramla Shija (NDL), Amen Isangi (DP), Fatma Ally (UMD), Emiliana Malema (CCK), Ibrahim Juma (CHAUMA) na Mvano Idd (ACT-Wazalendo).

**ACT YAKATA RUFANI**

Wakati huo huo, ACT-Wazalendo Jimbo la Shinyanga Mjini, imewasilisha barua ya kukata rufani kwa Afisa wa Uchaguzi Manispaa ya Shinyanga, kupinga mgombea wao Mvano Iddy kuenguliwa.

Awali msimamizi msaidizi wa uchaguzi mdogo Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga Timothy Andrew, alitangaza Mgombea huyo wa ACT Wazalendo kupitishwa kugombea Kata hiyo, atachuana na Mgombea wa CCM, Victor Mmanywa, lakini juzi majira ya saa 9 alasiri, akamtengua mgombea wa ACT-Wazalendo.

Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo Jimbo la Shinyanga Mjini, Omary Gindu, akizungumza na Nipashe jana baada ya kuwasilisha rufani yao kwa Afisa wa Uchaguzi Manispaa ya Shinyanga, Chalres Kafutila, alisema anaiomba NEC kutenda haki dhidi ya mgombea wao.



Mratibu wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Tanga kwenda Ohima nchini Uganda, Asiadi Mrutu, akizungumza na wadau mbalimbali kuhusu kujitokeza kuchangamkia fursa za mradi huo, wilayani Muheza jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## CHADEMA yadai polisi kuzingira ofisi kikao cha ndani

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

ZAIDI ya askari 10 baadhi yao wakiwa na silaha za moto wamedaiwa kuzingira ofisi za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Mbeya, katika kikao cha ndani cha viongozi wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA).

Tukio hilo limetokea jana na kuzua taharuki ikiwa imebaki siku moja Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini kufanya mkutano na wadau wa vyama vya siasa kwa lengo la kuondoa misuguano kati ya vyama hivyo na Jeshi la Polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, alisema hana taarifa za tukio hilo na wala hajatuma askari yeyote kwenda kwenye ofisi za chama hicho.

"Sijatuma wala kuagiza mtu kwenda huko kwa hiyo kama kuna mtu ambaye amekwenda kivyake vyake atajua mwenyewe," alisema Kamanda Matei. Mwenyekiti wa BAWACHA Mkoa wa Mbeya, Elizabert Mwakipesile, akizungumza na gazeti hili alisema jana saa 4:00 asubuhi wakati wakijiandaa na kikao, magari mawili ya polisi yalifika katika ofisi zao zilizopo eneo la Kadege, jijini Mbeya, moja lilisimama upande wa kushoto na jingine kulia huku baadhi ya askari wakiwa na silaha za moto.

Alisema, baadhi ya askari walishuka chini hali iliyozua hofu kwa kuwa vikao vya ndani vinaruhusiwa kama kawaida.

"Tulivyoona hayo magari ya polisi wakati tukiwa bado nje ya ofisi ilibidi tukawasiliana na Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote, ambaye alituambia tuingie ndani ya ofisi tuendelee na kikao kama kawaida na kuahidi atakuja eneo la tukio," alisema.

Mwakipesile alisema kikao hicho ambacho kilikuwa ni cha uratibu BAWACHA kwa lengo la kufanya tathmini zoezi la usajili wa wanachama kwa mfumo wa kidigitali kiliwakutanisha wenyeviti na makatibu wa majimbo saba ya uchaguzi ya mkoa huo. Hata hivyo, alisema baada ya polisi kuzingira ofisi hizo, saa moja baadaye waliondoka na kikao kikaendelea kama kawaida.

Alilitaka Jeshi la Polisi kuacha kuingilia shughuli za kisiasa kwa kuwa vikao vya ndani vya chama vinaruhusiwa kwa mujibu wa sheria.

Naye Joseph Mwasote, maarufu China, alisema anasikitishwa na mwenendo usiofaa wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya wa kufuatilia na wakati mwingine kuzuia mikutano ya ndani ya chama.

## Chongolo aonya wanaopinga ujenzi viwanda vya dawa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KATIBU Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, amewaonya watu wanaopiga vita uanzishwaji wa ujenzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba kijiji cha Idofi, mkoani Njombe.

Chongolo alitoa onyo hilo jana baada ya kutembelea na kukagua ujenzi huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 12.

"Niwahakikishie iwe jua au mvua hamna mtu atatia mkono kwenye hili, kiwanda kitajengwa na wakihitaji fedha nyingine za ziada njooni mimi nitakuwa daraja la kwenda kwa Rais," alisisitiza Chongolo.

Aliipongeza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa jitihada za kuanzisha viwanda vinne vya kutengeneza dawa pamoja na mipira ya mikono, ili kunusuru upotevu wa fedha zaidi ya Sh. bilioni 33 zinazopotea kuagiza dawa kutoka nje kwa mwaka.

"Hili litamaliza uchakachuaji wa dawa, zipo tulizokuwa tunaletewa kutoka nje zilikuwa zimebakia wiki mbili kuisha muda wake na fedha zimeshatumika, sasa hivi tutatengeneza dawa za miaka miwili mbele kwa uzuri na ubora ambao tutajiridhisha wenyewe na mambo yatatunyookea," alisema Chongolo.

"Tumetembelea huu mradi tumeridhishwa sana kwa sababu una matokeo chanya ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2020/25, tumeona maandalizi ya maeneo ya kuweka mitambo na mingine ipo bandarini kwa dhati kabisa tumpongeze Rais wetu kwa kuona umuhimu wa kuwekeza fedha kwenye miradi ya muda mrefu," alisema.

Naye Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema serikali imetumia Sh. bilioni 12 badala ya Sh. bilioni 18 zilizotarajiwa kutumikia kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa dawa.

Gwajima alisema serikali kupitia MSD imedhamiria kushusha gharama za dawa, vipimo na vifaa tiba kwa lengo la kuhudumia mwananchi mwenye kipato kidogo baada ya kujengwa kiwanda hicho.

"Kiwanda hiki kinaenda kuleta mapinduzi makubwa ya kuongeza uzalishaji wa dawa hapa nchini kwa asilimia 86, ili kuwezesha zahanati, vituo vya afya na hospitali kupata dawa na vifaa tiba kwa wakati," alisema Gwajima.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD), Meja Jenerali Gabriel Mhidze, alisema faida ya ujenzi wa kiwanda hicho ni kurahisisha upatikanaji wa dawa.

## TANGAZO




The Guardian

Nipashe
MWANGA WA JAMII

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuengua wagombea sio afya kwenye demokrasia

**AGOSTI 23,** mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akipokea taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka jana, aliitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuangalia sheria za uchaguzi ili zisitumike kuwanyima wagombea haki wakati wa uchaguzi.

Alisema masuala ya kiufundi, mathalani pale mtu anapokosea kuandika herufu za jina lake au za chama chake yasitumike kumnyima haki ya kushiriki uchaguzi.

Agizo hilo lilionekana kushusha pumzi kwa upinzani kwa kuwa walishangilia sana kama namna ya kufikisha ujumbe wa kilio chao cha muda mrefu, kwa kuwa katika uchaguzi huo na uchaguzi mbalimbali kabla ya hapo ukiwamo wa serikali za mitaa mwaka 2019 wengi walienguliwa kwa sababu hizo hizo, hivyo kuwaacha wa chama tawala (CCM) pekee wakipita bila kupingwa.

Umepita mwezi mmoja, wagombea 10 wa vyama vya upinzani walioomba ridhaa ya kugombea udiwani Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, wameenguliwa kwa madai ya kukosa sifa kwa kuwa kwenye fomu zao zilikuwa na kasoro.

Imeelezwa kuwa mgombea pekee wa CCM ndiye aliyepitishwa kwa kuwa fomu yake haikuwa na kasoro yoyote na alitimiza vigezo vyote muhimu. Tunafahamu kuwa maagizo ya Rais ni sheria na watendaji wa taasisi zote wanapaswa kuitekeleza. Hata hivyo, inashangaza kusikia katika hili bado mamlaka husika hususani NEC yenye jukumu la kusimamia uchaguzi kutochukua hatua za utekelezaji wa agizo la Rais la kuacha kuengua wagombea wa upinzani kwa sababu zile zile, huku mgombea wa chama kimoja akiachwa kwa sababu zile zile zilizotumika kwenye chaguzi nyingine.

Kimsingi, jambo hili halina taswira nzuri kwa jamii ndani na kimataifa kwa kuwa linazuia ushindani ulio sawa kwenye demokrasia, kwamba siku zote wanaokosea ni wa vyama vya upinzani ila wasiokosea ni wagombea wa chama tawala! Matukio haya yanaweza kuendeleza malalamiko yasiyo ya lazima ya baadhi ya watu kwenye jamii kuwa NEC haiko huru, kwa kuwa wasimamizi wa uchaguzi ambao ni wateule wa Rais, wanaegemea upande mmoja na kusahau wajibu wao wa kutengeneza mazingira ya ushindani kwa vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Malalamiko ya wagombea wa upinzani kuenguliwa ni ya muda mrefu na hutokea kwao kwa kuelezwa na wasimamizi wa uchaguzi kwamba fomu zao zimechelewa au zina kasoro mbalimbali zinazowafanya wakose sifa ya kuruhusiwa kugombea nafasi husika.

Jambo hili likitazamwa na sura tofauti tofauti linaweza kuonyesha kuwa huenda vyama haviwaandai wagombea wake na kuwaelekeza namna ya kujaza fomu.


Tunaona kwamba makamishna na watendaji wa NEC wanawajibika sasa kuhakikisha kwamba maagizo ya Rais Samia yanatekelezwa ipasavyo, vinginevyo hali hiyo inaweza kutafsiriwa vibaya na umma.

Kuacha hivi kunaweza kusababisha wadau wa uchaguzi na umma kwa ujumla kupoteza imani kwa NEC na matokeo yake kupunguza idadi ya wapigakura, kuongeza malalamiko ya wapinzani na kutengeneza mazingira kuwa wao hawatendewi haki.

Ni muhimu sana wasimamizi wa uchaguzi wakatambua kuwa wanapaswa kufanyakazi kwa mazingira yenye uwanja sawa wa ushindani kuliko kumtengenezea mmojawapo mazingira ya ushindi kabla ya uchaguzi kufanyika, kwa kuwa ikiwa wote wameenguliwa maana yake aliyebaki anatangazwa kuwa mshindi. Ni muhimu maswali magumu yawe na majibu sahihi na kusiwe na majibu rahisi kwa maswali magumu, kwa kuwa jamii ya sasa siyo ya miaka ya 60, bali inauelewa wa kuchanganua, kupima na kufanya maamuzi sahihi kwa kile wanachoona ni sahihi.

Ni muhimu NEC ikafanyia kazi maagizo ya Rais kwa kuwa kama mwanasiasa na mkuu wa nchi ameona kasoro ilipo na inapaswa kurekebishwa ili kutenda haki kwa wote, na vyama kutimiza wajibu wao kuondoa malalamiko yasiyo ya lazima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wagombea wote upinzani Shinyanga kuenguliwa kunavyozidisha maswali

Na Sabato Kasika

**UCHAGUZI** mdogo wa diwani wa kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao baada ya kifo cha David Nkulila, umeanza kwa vimbwanga vya washiriki wote wa upinzani kuangukia pua, kwa maelezo kuwa hawakukidhi vigezo.

Diwani Nkulila, aliyekuwa pia Meya wa Manispaa ya Shinyanga, alifariki dunia Agosti mwaka huu na sasa uchaguzi wa kuziba pengo lake utafanyika Oktoba 9 na ndivyo mchakato unavyoanza.

Waliojitokeza, lakini wakaenguliwa na kumbakiza mgombea wa CCM pekee Victor Mmanywa, wanatoka vyama vya Demokrasia Makini, ADC, SAU, NLD, UMD, CCK, CHAUMMA, NRA, DP na ACT-Wazalendo.

Kuenguliwa kwa wagombea 10 kutoka vyama vya upinzani, kuwania nafasi hiyo kunatokana na kile kinachoelezwa na msimamizi wa uchaguzi huo kuwa ni kutokidhi vigezo vya kugombea udiwani kwenye uchaguzi huo utakaofanyika Oktoba 9, mwaka huu.

Hayo yanafanyika Shinyanga, wakati Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa ameshatoa maelekezo kwamba ni muhimu sheria zikazingatiwa ili zisitumike kuwanyima watu haki kwa madai kuwa wanashindwa kuandika au kokosea majina yao.

Rais alisema mtu anapokosea kuandika baadhi ya herufi za jina lake au za chama chake, kisiwe kigezo na kwamba mipango ingewekwa vizuri ili asienguliе, lakini akawataka wagombea nao kuwa makini wanapojaza fomu.

Ni wakati akipokea ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020 iliyowasilishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kutoa wito huo ili kwamba wagombea waweze kuchukuana kwenye kinyang'anyiro, badala ya kuwapo malalamiko ambayo wakati mwingine si ya lazima.

Rais aliwataka wagombea kuwa makini wanapojaza fomu ili wasiache nafasi ambayo itawafanya wapinzani wao kuitumia kuwaengua katika kinyang'anyiro.

Alichosema kilitakiwa kuwa somo hata kwa wanasiasa waliojitokeza kuwania udiwani wa Kata ya Ndembezi, ili kwamba makosa yasijirudie kama ambavyo yamekuwa yakifanyika katika uchaguzi mbalimbali.

Kwa mfano, sababu ya kuenguliwa mgombea wa ACT-Wazalendo aliyekuwa ameteuliwa rasmi na kupewa barua ya uteuzi imeelezwa kuwa hakujaza fomu namba 8 (c) na namba 10 (c) na kuzirudisha NEC kwa wakati.

Hata hivyo, Katibu Mwenezi wa chama hicho Shinyanga Mjini, Omary Gindu, anasema mgombea wao alikuwa tayari amepewa barua ya uteuzi, lakini wa CCM akamwekea pingamizi, Mvano Idd, ambaye atakata rufani, ili jina lake lirejeshwe kwenye kinyang'anyiro.

Mapingamizi kama hayo yalitokea katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, ambayo huenda yangekuwa fundisho kwa wagombea ili wawe makini katika ujazaji wa fomu za kuwania udiwani au ubunge.

Lakini kama ni makosa ambayo aliyagusia Rais Samia na kutaka yarekebishwe, ingependeza wasimamizi wakasaidia kuwarekebisha wagombea kwenye kasoro hizo za kawaida, ili hatimaye wapate nafasi ya kushiriki kwenye kinyang'anyiro.

Hatua hiyo, inaweza kusaidia kuleta hamasa katika uchaguzi badala ya watu kupita bila kupingwa, hali ambayo wakati mwingine inaweza kusababisha wagombea na kudhani hawana nafasi ya kuchaguliwa.

Mbali na hilo, hata kelele za mara kwa mara za wapinzani ambazo zinajitokeza wakati wa uchaguzi kudai kuenguliwa, kunyimwa fomu au kutopokelewa fomu zao, zinaweza kutapungua

Pamoja na hayo, upinzani utakuwa umekosa hoja ambazo huelekezwa kwa wasimamizi wa uchaguzi kuwa mamia ya wagombea wao huenguliwa ili kuwapa ushindi wa 'mezani' wagombea wa CCM.

## HABARI KITAIFA

### Wateja waguswa ubunifu huduma Benki ya Amana

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Benki ya Amana wamebainisha kufurahia matumizi ya programu ya kidigitali ya benki hiyo ijulikanayo kama Amana Bank App.

Huduma hiyo inawezesha wateja kufanya miamala na kupata huduma za kibenki mtandaoni ambayo ilizinduliwa hivi karibuni.

Baadhi ya wateja wa benki hiyo walipohojiwa kuhusu huduma hiyo, walisema programu hiyo ni ubunifu mkubwa katika kurahisisha wateja maisha, pia ina upekee wake kutokana na kuwalenga pia wateja wanaohitaji huduma za kibenki za Kiislamu.

Mkazi wa Dodoma, Hassan Mabuye, ambaye ni mmoja wa watumiaji wa huduma hiyo, alisema Amana Bank App ni huduma inayorahisisha maisha kwa kuwa anaweza kufanya miamala ya malipo kupitia simu yake ya mkononi akiwa mahali popote na wakati wowote na ni rahisi kuitumia, ya haraka na salama.

Jira Athuman alisema anaifurahia huduma hiyo na imekuwa msaada mkubwa kufanya shughuli zake.

"Amana Bank App inaniwezesha kupata huduma za kibenki kidigitali kama vile kufanya malipo, kuhamisha fedha, kulipia bili na kufanya malipo mtandaoni, kupokea taarifa za benki na kupokea habari juu ya huduma zinazotolewa na benki kama mikopo, viwango vya ubadilishaji wa kigeni na hata kulipia huduma mbalimbali kama malipo ya serikali na huduma za bima," alisema.

Mteja mwingine wa benki hiyo Natty Natty, alisema anaitumia huduma hii kupitia namba yake ya Masterpass QR kulipia huduma mbalimbali ikiwamo kulipia mafuta ya gari, maduka ya vyakula, migahawa, maduka ya dawa, hospitali na vituo vingi vinavyotoa huduma.

# Mawaziri waanika mkakati kuwapanga wamachinga

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imejipanga kuwa na idara mahususi ya kushughulikia viwanda, biashara na uwekezaji katika halmashauri zote nchini sambamba na kuwapo kwa dawati maalum litakalotatua kero zote za wamachinga.

Lengo ni kutekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ambayo kwamba ni lazima wawapange wafanyabiashara wadogo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mpango wa kuwapanga wamachinga kwenye vibanda 652 vilivyojengwa katika Soko Kuu la Chifu Kingalu Manispaa ya Morogoro kwa kuchukua wafanyabiashara 468 vyenye thamani ya shilingi milioni 81.7.

Alisema kwao TAMISEMI maelekeo ya Rais Samia yamewapa nguvu, ari na moyo wa kuhakikisha wamachinga wanapangwa nchi nzima na aliushukuru Mkoa wa Morogoro kwa kuanza na ameahidi kuwaunga mkono kwani ni mkoa wa mfano ambao unapaswa kuigwa.

Mwalimu alisema wameanza kufanya mabadiliko kwa kufufua idara ya uendelezaji miji na vijiji ili kuwabana maofisa mipango miji na vijiji kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Alisisitiza viongozi wa mikoa kuhakikisha wanatatua changamoto ya wafanyabiashara wadogo kwa kuanza kuhakikisha wanasajili biashara zao, ili wapate fursa zinazotolewa na serikali.

Pia alisisitiza kila halmashauri kuhakikisha kunakuwa na maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo, ambayo yanapaswa kuendelezwa kwa sababu vijana bado wanatoka vijijini kwenda mijini.

"TAMISEMI kwa kushirikina na Wizara ya Viwanda na Biashara tutahakikisha tunapunguza mikakati ya vijana kutoka vijijini kuja mijini kwa sababu ujio wao sasa unaongezeka kwa kasi na mpaka sasa jijini Dar es Salaam pekee wanaingia vijana 300 zaidi kila mwezi," alisema Waziri Ummy.

"Nazitaka halmashauri zote nchini kusimamia ipasavyo utengaji na kuendeleza maeneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara ndongo na tunamhakikishia mheshimiwa Rais tutalisimamia hili," alisema.

Alisema kwa mujibu wa taarifa kutoka Idara ya Takwimu, wafanyabiashara wadogo wapo takribani milioni 31 nchini ambapo Watanzania wote ni milioni 60 na hiyo inaonyesha wazi kuwa wafanyabiashara hao wapo wengi nchini.

Aidha alisisitiza halmashauri kutoa mikopo ya riba nafuu zitakazowasaidia kukuza mitaji ya wamachinga hao kwani biashara bila mtaji haiwezi kufanyika.

Naye Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, aliwashauri mawaziri wenzake kutoka nchi za Afrika kwenda mkoani Morogoro kujifunza namna ya utatuzi wa changamoto za wamachinga.

Waziri Mkumbo alitoa wito kwa serikali na wafanyabiashara wanaokabidhiwa mabanda kusimamia na kutoyapuuza makubaliano waliyowekeana kwa sababu nchi inaendeshwa kwa utawala wa sheria na sheria yoyote inayowekwa haipaswi kuvunjwa ili kuhakikisha usalama, amani na mshikamano vinaonekana kwa wote.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, alisema mpango wa halmashauri ni kutengeneza vibanda vya wafanyabiashara wadogo takribani 800.

Alisema awali walikabiliwa na changamoto za wamachinga katika Halmashauri ya Morogoro ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa wafanyabiashara juu ya masuala ya biashara na wafanyabiashara kufanya shughuli zao kiholela hasa kwenye maeneo yaliyozuiliwa kwa mujibu wa sheria.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema kabla ya ujenzi wa vibanda hivyo alikaa na wafanyabiashara na kukubaliana kutumia eneo la maegesho kwenye soko la Kingalu kwa ajili ya kujenga vibanda vya kufanyia biashara ambavyo kwa sasa vimekamilika.

Mwenyekiti wa Machinga Mkoa wa Morogoro, Faustine Francis, alipongeza uongozi wa mkoa na wilaya kwa kuwajengea vibanda vya biashara na kwamba wameonyesha kuwajali.




LAWS OF LOVE IS A TELENOVELA ABOUT PROFESSIONAL LAWYERS WORKING FOR A LEGAL FIRM CALLED VEGA. THE STORY EVOLVES AROUND LOVE, JEALOUSY, GREED, HATRED AND BETRAY WHEN THE LAWYERS MIX LOVE WITH PROFESSIONAL WORK.

DON'T MISS THIS CAPTIVATING TELENOVELA, STARTING ON 5TH OCT 2021 CAPITAL TELEVISION.



TAJIRI NA BILIONEA LEON CARVAHAL AJIKUTA MLENGWA WA WABAYA WAKE, AMALIZWA KIKATILI SIKU YA HARUSI YAKE, ROHO YAKE YAJITOKEZA UPYA KWA CHINO VALDES KIJANA MTUKUTU NA MHALIFU ANAYEOGOPEKA AMBAYE NAYE ALIMALIZWA KWA HUKUMU YA KITI CHA UMEME. NA MWISHO PROFESA BETRAN CAMACHO NAE APATA AJALI MBAYA YA GARI NA KUFARIKI DUNIA. HAWA WOTE WATATU WAFARIKI MUDA MMOJA, MAENEO, VYANZO NA MAZINGIRA YA VIFO VYAO NI TOFAUTI. JE, NI NANI WAHUSIKA WA VIFO HIVI VITATU?.

LOVE TO DEATH KUANZIA TAREHE 4 OKTOBA SAA 4:10 USIKU ITV PEKEE!!

ITV

# Vyuo vya uuguzi, ukunga visivyo na sifa kufungwa

**Na Moshi Lusonzo**

SERIKALI imetangaza kufanya uchunguzi na kuvifunga vyuo vya uuguzi na wakunga visivyo na sifa ambavyo vinashusha viwango vya taaluma hiyo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Baraza jipya la Wauguzi na Wakunga mjini Kibaha mkoani Pwani, juzi, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dorothy Gwajima, alisema kumekuwa na utitiri wa vyuo vinavyotoa mafunzo ya fani hizo, lakini vingi havina sifa na kuzalisha watu wenye weledi na maadili.

Alisema katika ngazi ya utumishi wa afya, kada ya uuguzi na wakunga ni zaidi ya asilimia 60, hivyo wana umuhimu katika kulinda afya za wananchi kulingana na miongozo, sheria na kanuni.

"Baraza linatakiwa kuwa na umakini katika kuongeza kiwango, wizara itafanya uchunguzi na kuondoa utitiri wa vyuo visivyo na sifa na nyinyi mnatakiwa kufuta leseni kama ikionekana kuna ulazima," alisema Waziri Gwajima.

Akizungumzia watumishi wanaokiuka maadili na miongozo ya kitaaluma, alitaka chombo hicho kutowavumilia badala yake kuwapa adhabu Kali.

" Natangaza rasmi kama kuna mtu kafanya kosa na baraza lenu likamchukulie hatua, asije ofisini kwangu kuomba msaada wa kusamehewa," alisema.

Waziri huyo aliwapongeza wajumbe wa baraza liliopita kwa kazi nzuri, hasa kazi ya uboreshaji wa utendaji kazi kwa kuanzisha kanzidata, ambayo inarahisisha kutambua watumishi wa kada hizo.

Mwenyekiti mpya wa baraza hilo, Ziada Sellah, alimhakikishia Waziri Gwajima kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo ya taasisi hiyo pamoja na kuendelea na kazi nzuri iliyoachwa na wajumbe wa zamani.

Alisisitiza baraza hilo litahakikisha linaongeza viwango kwa kuhakiki utendaji kazi kwa vyuo kwa kuangalia kama vinakidhi utoaji wa mafunzo ya taaluma hiyo.



Magari yakipita kwa tabu katika Mtaa wa Sikukuu, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na msongamano mkubwa wa wafanyabiashara wadogo maarufu machinga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbarawa ataka daraja Wami kujengwa saa 24

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amemwagiza mkandarasi anayejenga daraja la Wami kufanya kazi saa 24, ili kukamilisha kazi kwa wakati.

Prof. Mbarawa alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara kukagua maendeleo ya daraja hilo linalojengwa na Mkandarasi Power Construction Corporation ya China.

Alisema ujenzi wa daraja hilo ulianza Oktoba 2018 na matarajio ilikuwa kukamilika mwezi Septemba 2021 limechelewa kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo mvua na ugonjwa wa Uviko-19.

Alimsisitiza mkandarasi pia kujenga daraja hilo kwa ubora unaotakiwa ili lidumu kwa muda mrefu na ifikapo Novemba 2022 ujenzi uwe umekamilika. Waziri Mbarawa alisema daraja la awali lenye urefu wa mita 88.75 lilijengwa mwaka 1959 na kwasasa lina uwezo mdogo wa kupitisha magari yanayoenda mikoa ya Kaskazini na nchi za jirani kutokana na ongezeko la magari.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Pwani (TANROADS), Mhandisi Andrea Kasamwa alisema daraja hilo hadi kukamilika litatumia Sh. bilioni 72.

Mhandisi Kasamwa alisema daraja hilo jipya litakuwa na urefu wa mita 510 na upana wa mita 11.85 linajengwa umbali wa mita 670 pembeni ya daraja la zamani.

Alisema mkandarasi amewasilisha sababu za kimkataba nyongeza ya muda wa ujenzi kufika mwezi Novemba 2022.

Alisema kazi hiyo inasimamiwa na kampuni mbili ya Ilshin ya Korea na Advanced Engineering Solution ya Tanzania.

Kasamwa alisema maendeleo ya mradi hadi sasa yamefikia asilimia 61.4 na muda wa mradi uliopita hadi sasa ni miezi 35.

# Hisa za NICOL zaongezeka DSE

**Na Joseph Mwendapole**

HISA za Kampuni ya NICOL (National Investments PLC) zimeendelea kufanya vizuri katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), ambapo zimepanda kutoka Sh. 170 hadi Sh. 250 kwa hisa moja.

Kwa mujibu wa taarifa za mahesabu ya NICOL, faida ya nusu mwaka imekua kwa asilimia 68 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2020.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa NICOL, Erasto Ngamilaga, aliliambia gazeti hili kuwa gharama za uendeshaji za kampuni ya NICOL zimepungua kwa zaidi ya asilimia 37 ikilinganishwa na msimu uliopita.

Alisema faida hiyo imetokana na ongezeko la mapato ya msimu wa nusu mwaka wa 2021 yaliyotokana na faida ya uwekezaji katika kampuni mbalimbali pamoja na riba za hati fungani.

Ngamilaga alisema kutokana na mafanikio hayo, bodi na menejimenti ya kampuni ya NICOL zinaendelea kuchukua hatua kuongeza mapato na kupunguza matumizi, hatua ambazo zitawezesha kuendelea kuimarisha uwekezaji na kuongeza malipo ya gawio kwa wanahisa wake.

"Tunafanya vizuri na tunaahidi kuendelea kufanya vizuri zaidi na wanahisa wetu watarajie kuona bei ya hisa za kampuni katika soko la hisa DSE zinaendelea kuimarika, sambamba na kuongezeka kwa malipo ya gawio kwa wanahisa wetu," alisema.

Alisema mpango mkakati wa kampuni hiyo ni kutawanya uwekezaji katika maeneo yenye kuleta tija kwa wanahisa, ambapo mpaka tarehe ya mahesabu ya kampuni hiyo wamewekeza kwenye dhamana za serikali zaidi ya Sh. bilioni 7.6 na matarajio ni kuongeza uwekezaji kwenye dhamana za serikali kufikia hadi Sh. bilioni 15 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2021.

Alisema uwekezaji huo utasaidia kuboresha mapato kwa wanahisa kwa kuongeza gawio na kuongeza thamani ya kampuni na pia kuimarisha bei ya hisa kwenye DSE.

**"Tunafanya vizuri na tunaahidi kuendelea kufanya vizuri zaidi na wanahisa wetu watarajie kuona bei ya hisa za kampuni katika soko la hisa DSE zinaendelea kuimarika, sambamba na kuongezeka kwa malipo ya gawio kwa wanahisa wetu," alisema.**

HABARI KITAIFA

## Chuo cha Ardhi Tabora kuongeza wataalamu ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) umesema umepiga hatua kubwa ikiwamo kuongeza idadi ya wanafunzi ili kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa ardhi nchini.

Umebainisha kuwa katika mpango kabambe wa miaka 10 (2010-2020) kimeongeza udahili mwaka hadi mwaka, idadi ya wanafunzi ikiongezeka kutoka wanafunzi 146 mwaka wa masomo 2009/2010 hadi kufikia 1,414 mwaka 2020/21.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Donald Rweramila, alisema jana kuwa tangu kilipoanzishwa mwaka 1979, kilikuwa kikiongeza udahili wa wanachuo kulingana na miundombinu iliyokuwapo.

Alibainisha kuwa mwaka 2009, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilibuni mpango kabambe wa miaka 10 uliolenga kupanua chuo hicho kwa kuongeza miundombinu, kuongeza vitendea kazi ambavyo vilileta ongezeko la idadi ya wana chuo kutoka 146 mwaka 2009/10 hadi 1,414 mwaka 2020/21.

Kaimu Mkuu huyo wa Chuo alisema chuo kimefanikiwa kuandaa na kuboresha mitaala yote kwa kufuata mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili tuzo zitolewazo na chuo hicho ziwe na kiwango cha ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa.

Alisema wamefanikiwa kupata usajili na ithibati kamili kutoka NACTE ya kutoa mafunzo ya Sekta ya Ardhi katika ngazi ya astashahada na stashahada.

"Wahitimu katika ngazi ya stashahada wenye ufaulu stahiki wanazo sifa za kujiunga na masomo ya shahada ya kwanza katika chuo kikuu chochote ndani na nje ya nchi kinachofundisha taaluma za Sekta ya Ardhi au zinazohusiana," alisema.

Aliongeza kuwa chuo pia kimeboresha mfumo wa upatikanaji wa majisafi kwa matumizi ya wanachuo katika bweni jipya kwa kujenga tangi la kuhifadhi maji chini ya ardhi lenye ujezo wa lita 200,000.

"Chuo kimeweza kuboresha mfumo wa umeme kwa kuingiza umeme wa njia tatu na kusimika transfoma ndani ya eneo la chuo ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la matumizi ya umeme," alisema na kubainisha kuwa wamenunua jenerata kubwa lenye uwezo wa kuhudumia eneo lote la chuo wakati wa upungufu au hitilafu ya umeme unaotolewa na Shirika la Umeme (TANESCO).

Alisema chuo hicho pia kimefanikiwa kuanza ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua watumiaji 360 na kompyuta 50 kwa wakati mmoja.

"Chuo kimefanikiwa kusimika mfumo wa udahili wa wanafunzi ambao umebuniwa na kusimikwa na Chuo Kikuu Ardhi – Dar es Salaam.

"Mfumo huu shirikishi unasaidia kurahisisha usajili wa wanachuo, kutunza kumbukunbu sahihi za wanachuo, utangazaji wa matokeo ya mitihani na kudhibiti ulipaji wa ada za masomo kwa wanachuo," alisema.

Alibainisha chuo kimefanikiwa kuendelea kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali iliyopo chuoni ikiwa ni pamoja na ofisi za watumishi, madarasa, mabweni ya wanachuo na ununuzi wa samani.

Tangu chuo kilipoanzishwa mwaka 1979 hadi mwaka 2017, kimefanikiwa kutoa jumla ya wahitimu 3,303.

# Wagomea malipo ufuta na korosho kupitia simu

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKULIMA wa korosho na ufuta mkoani Lindi wamekataa utaratibu wa kulipwa fedha zinazotokana na mauzo ya mazao yao kupitia mitandao ya simu.

Wamedai wengi hawajapata elimu ya kutosha, huku wengine wakiwa na mikopo katika benki mbalimbali, hali itakayowavuruga akili zao.

Tamko la kukataa utaratibu huo limetolewa na wakulima hao kupitia viongozi wao wa Vyama vya Msingi na Ushirika (Amco's) katika mkutano wa wadau uliofanyika mjini Lindi.

Wakulima hao wametoa tamko hilo kutokana na viongozi wa mitandao ya simu ya Tigo, Airtel na mengineyo kuwashawishi wakulima wawe tayari kupokea fedha wanazolipwa, baada ya kuuza mazao kuanzia msimu wa mwaka huu kupitia simu zao za mikononi, badala ya kwenda benki.

Aidha, viongozi hao walidai kupokea malipo kupitia mtandao wa simu ni rahisi na salama zaidi kwa fedha zao na kupunguza muda wa kutembea kufuata malipo yao benki.

Wakijibu maelezo ya viongozi hao wa mitandao ya simu, wakulima hao kupitia viongozi wao wa Amco's, Said Rashidi Mkwata,(Mnazi Mmoja) na (Mnari Amco's) na Salum Ahmadi Kazembe (Mnari Amco's) walisema hawapingani na maelezo yao, kwani una faida zake.

Pia, walisema wanachama wao ni wakulima na wanazo simu wanazozitumia kwa mawasiliano, hivyo itakuwa ni vizuri iwapo kwanza wakawafuata kwenye maeneo yao kuwapata elimu, badala ya kuwavamia kupitia mikutano ya wadau.

"Mheshimiwa mwenyekiti, mume anapotaka mchumba ajitokeze kwa wazazi wake, sio kumkuta njiani na kumtangaza eti mumeo, haiendi hivyo," alisema Kazembe.

"Hawa mabwana wa mitandao tunakutanao hapa leo katika mikutano huu, fanyeni kama wenzenu wa mbenki wanawafuata wateja huko huko vijijini na kuwapa elimu," alisema Rashidi.

Said Rashidi Mkata, ni makamu mwenyekiti wa Chama cha Msingi na Ushirika Mnazi Mmoja alisema wakulima wengi wana mikopo kutoka benki mbalimbali, hivyo mpango huo utakwamisha vyama kulipa madeni kwani itakuwa vigumu wakulima kurejesha fedha walizokopa katika taasisi hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Rashid Telack, akizungumza katika mkutano huo wa wadau wa korosho na ufuta, alizitaka kampuni za simu kwenda kwa wakulima na kuwapa elimu, ikiwamo umuhimu wa kulipwa kupitia mitandao yao simu zao.



Mwezeshaji Prince Bagenda (kulia), akizungumza wakati wa semina ya uelewa kwa waandishi wa habari katika kuripoti mradi wa bomba la mafuta kutoka Ohima nchini Uganda kwenda Tanga, iliyoandaliwa na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Equator Communications Ltd, kwa kushirikiana na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), jijini Dar es Salaam jana **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wenye matatizo ya mgongo wazi, kichwa kikubwa waomba msaada

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha wazazi wenye watoto walio na ulemavu wa vichwa vikubwa na mgongo wazi Tanzania (ASBAHT), kimesema ifikapo Oktoba 22, mwaka huu, kinatarajia kufanya maadhimisho ya watu wenye matatizo hayo kusaidia watoto 300.

Lengo la msaada huo ni kugharamia mifaa tiba na uchunguzi wa matibabu kwa watoto zaidi ya 300 wenye ugonjwa nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, jijini Dar es Salaam , Ofisa Utawala wa Chama hicho, Santos Chuwa alisema maadhimisho hayo hufanyika kila mwaka na kwamba kwa mwaka huu yatafanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja kitaifa.

Alisema kwa mwaka huu maadhimisho hayo wameyapa jina la matembezi ya hisani na kwamba mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu.

Kwa mujibu wa Chuwa, katika kufikia siku hiyo kutakuwa na shughuli mbalimbali za kijamii kama uchangiaji damu, kuhamasisha Watanzania kuchangia fedha za matibabu, kukagua mabanda, pamoja na kuzindua mpango endelevu wa watoto wenye vichwa vikubwa wakishirikiana na taasisi ya Mifupa MOI

"Tunaishukuru MOI kwa msaada mkubwa ambao mara nyingi wamekuwa wakitupatia kama vile kutoa msamaha wa matibabu wakati mwingine watoto wanatolewa kabisa gharama za matibabu,"alisema Chuwa.

Vile vile, aliiomba serikali kusaidia upatikanaji wa mipira maalumu kwa kwa kusambaza mlundikano wa maji kichwani iweze kupatikana kiurahisi, ili kusadia matibabu ya wagonjwa hao. Naye, Mratibu wa chama hicho, Hidaya Alawi alisema ifikapo Oktoba 25, mwaka huu watakutana na wadau mbalimbali wakiwamo wawakilishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wakuu wa wilaya zote Mkoa wa Dar es Salaam na viongozi wa dini.

"Siku hiyo tutaweza kufahamu njia na mbinu mbadala ambazo zitatumika kwa lengo la kuwasaidia wagonjwa hao ambao vifaa vyao mara nyingi vimekuwa havipatikani kiurahisi, tunaomba Watanzania watuunge mkono tuweze kuwasaidia,"alisema.

# Watumishi wasimamishwa madai kupoteza mapato ya halmashauri

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara, Elias Ntiruhungwa amewasimamisha kazi kwa muda usiojulikana wahasibu watatu wa halmashauri hiyo kwa makosa ya kughushi vibali na risiti za halmashauri kwa lengo la kujipatia fedha ambazo ni mapato ya halmashauri.

Alifanya uamuzi huo jana kwenye kikao maalum na watumishi hao kwa lengo la kupeana maelekezo ya uadilifu katika kazi za serikali.

Alisema halmashauri imekuwa ikipambana katika kukusanya mapato yake ya ndani kupitia vyanzo vyake vya mapato ili fedha hizo ziweze kutumika katika uketekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Katika bajeti yake halmashauri imetenga kiasi cha Sh. milioni 600 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hivyo kama mapato yanapotea hatafumbia macho mtumishi yeyote.

Alisema watumishi hao ni wahasibu watatu wa halmashauri hiyo ambao wamebainika kuwa na tabia ya kughushi vibali pamoja na risiti mbalimbali kwa lengo la kutaka kujipatia fedha kinyume cha taratibu za kazi.

Ntiruhungwa alisema watumishi hao wamekuwa wakichapisha nyaraka zao binafsi kana kwamba wamekuwa wakisafirisha mazao wakati hakuna wafanyabiashara ambao wanawapatia vibali na risiti hizo, na kwamba viwango vya fedha ambazo wamekuwa wakiandika kwenye vibali, hivyo hizo fedha wamekuwa wakiziingiza kwenye mifuko yao.

Alisema kuwa alifanya uchunguzi wa kufuatia hali ya mapato ya halmashauri kwa siku tatu mfululizo ili kubaini kwanini mapato yamekuwa yakipotea ndipo alipobaini kuwa mapato mengi yanapotea na halmashauri kukosa fedha.

Ntiruhungwa aliwataja wahasibu hao watatu ambao amewasimisha kazi kwa muda usiojulikana kupisha uchunguzi ni Liydia Barnabas, Ibrahim Bingwe na Semakweli Kassim.

Alisema hata hivyo, hadi sasa hakijafahamika kiasi cha fedha ambazo zimepotea.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi (wa nne kulia), akisikiliza maelezo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka kwa mtaalamu wa kampuni ya YapiMerkezi ya Uturuki juzi, jijini Dar es Salaam. Watendaji wakuu wa TCB, ambayo ni mshiriki wa kimkakati kwenye mradi huo, wako katika ziara ya kushuhudia maendeleo ya utekelezaji wake na kujionea ukubwa wa uwekezaji unaofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau ikiwamo benki hiyo. Jana viongozi hao walikuwa Morogoro na watamalizia ziara hiyo Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu kukatika umeme zaanikwa

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema sababu ya kutokuwapo nishati hiyo kwenye maeneo mengi hususan Dar es Salaam, hakuepukiki na kwamba kunatokana na mchakato unaoendelea wa kubadilisha nguzo na kusimikwa za zege.

Limesema ukataji umeme hufanyika kwa awamu kulingana na kanda na kwamba kwa siku nguzo zinazobadilishwa ni 50 hadi 100 pia muda wa kukata umeme ni kuanzia saa tatu asubuhi hadi 11 jioni.

Meneja Mwandamizi wa TANESCO Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, Mhandisi Hassan Said, akizungumza katika moja ya redio nchini kuhusu tatizo la kukosekana nishati hiyo hasa majira ya asubuhi hadi jioni, alisema imeundwa timu maalumu kwa ajili ya kuanya shughuli hizo kila eneo.

"Ni kweli tunazima umeme ili kufanya hiki. Ni uchungu wa uzazi ambao mwisho wake ni furaha. Zipo njia kubwa ambazo zinasambaza umeme zilizo na feeder 216 zenye msongo wa volti 33,000 na mwingine ni volti 11,000. Tunapofanya matengenezo tunahakikisha eneo kubwa haliathiriki na umeme," alisema Hassan.

Alisema mchakato wa kubadili nguzo za zege hufanyika mara moja au mbili kwa wiki, na kwamba mpango huo ni kuondoa nguzo za zamani ambazo nyingi zilikuwa zimeoza.

"Haikubaliki muda wa umeme kurudishwa nje ya ule uliowekwa kwenye ratiba. Ila kuna suala la kiusalama na kabla ya kurudisha umeme. Maeneo ya Dar es Salaam ni kati ambayo yanaingiza mapato makubwa kwa shirika, kunapokosekana umeme nasi tunaathirika," alisema Hassan.

## Mila, desturi zaendelea kuchochea ukatili kijinsia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kasper Mmuya, ameyataka mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani Shinyanga kushirikiana na serikali kumaliza tatizo la mila na desturi kandamizi, ambalo limeendelea kuchochea matukio ya ukatili wa kijinsia.

Alibainisha hayo juzi mkoani Shinyanga, kwenye kikao cha wadau wa ulinzi na usalama kwa wanawake na watoto kujadili utekelezaji wa mpango mkakati wa Taifa wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA).

Alisema mila na desturi kandamizi, bado zimeendelea kuwa changamoto mkoani Shinyanga na kusababisha kuendelea kuwapo kwa matukio ya kutatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

"Mila na desturi kandamizi katika maeneo mengi nchini, zimeendelea kuwa kikwazo kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, naomba mashirika mshirikiane na serikali kutokomeza mila na desturi kandamizi ndani ya jamii, ndipo tutafanikiwa kumaliza ukatili," alisema Mmuya.

"Nitumie pia fursa hii kuiomba jamii, iachane na masuala ya mila na desturi kandamizi, na kutomaliza kesi kienyeji za matukio ya ukatili, zikiwamo mimba na ndoa za utotoni, ili wahusika wafungwe jela, na kutokomeza kabisa matukio haya na wanafunzi kutimiza ndoto zao," aliongeza.

Naye mratibu wa masuala ya jinsia kutoka Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mwajina Lipinga, aliwataka waratibu wa MTAKUWWA kutekeleza majukumu yao ipasavyo pamoja na kushirikiana na mashirika kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Mratibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Wanawake na Watoto mkoani Shinyanga, Tedson Ngwale, alisema mkoa huo unafanya juhudi kubwa kupambana na matukio ya ukatili, ambapo wamefikia hatua ya kuzindua mpango mkakati wa miaka mitano kutokomeza matukio hayo.

Nao wajumbe (MTAKUWWA), wameishukuru serikali kwa kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutatua changamoto zilizopo ndani ya jamii yakiwamo matukio ya ukatili wa kijinsia.

**Alisema mila na desturi kandamizi, bado zimeendelea kuwa changamoto mkoani Shinyanga na kusababisha kuendelea kuwapo kwa matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake.**

Watanzania tatizo si utawala bora, shida kubwa ni uchumi

Ukurasa 12





Ukurasa 14

**VLADIMIR PUTIN**
**Miongo miwili madarakani, ataishi ikulu hadi 2036**

siasa
JUMATANO SEPTEMBA 22, 2021
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# Ziara ya Chongolo, timu yake inavyowabana mubashara viongozi wanaolalamikiwa

- Yaanza na Byabato vipi kukatika umeme ovyo
- Shaka amvaa waziri kwa simu 'live' kieleweke

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa Mtwara**



Shaka Hamdu Shaka (aliyenyanyua mikono ndani ya gari) pamoja na mabosi wa CCM, wanaozunguka mikoani kukiimarisha chama ngazi ya mashinani. **PICHA: BEATRICE SHAYO.**

ZIARA ya wajumbe wa Sekretarieti ya CCM, mikoa ya Kusini imeibua vicheko na kuacha furaha kwa wananchi baada ya viongozi wa chama kuwaweka kitimoto viongozi wasiomaliza kero na kuwataka kujibu malalamiko ya wananchi, dhidi yao.

Katika moja ya matukio hayo, wajumbe wa sekretarieti ya CCM wanawahoji watendaji wanaolalamikiwa na wananchi akiwamo Naibu Waziri wa Nishati Stephen Byabato, akitakiwa kueleza kero za kukatika umeme kila wakati inakwisha lini.

Ujumbe huo, ukiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, umefanya ziara katika maeneo mbalimbali mikoani Lindi, Mtwara, Ruvuma na Njombe.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, wakati akizungumza na wananchi wa mashina namba moja la Nambambo na shina la Namatula lililopo Nachingwea mkoani Lindi , kupokea malalamiko ya umeme kukatika ovyo, tena kila wakati na ubovu wa barabara.

Viongozi hao wako kwenye ziara inayolenga kuimarisha chama mashinani pamoja na kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025.

Wanapokutana na viongozi wa chama, wananchi wanaeleza kukatika huko kumewasababishia hasara kwa kuharibu vifaa vyao kama majokofu, runinga na redio.

Shaka anasema CCM na serikali haitavumilia changamoto za kuwaumiza wananchi, ndiyo maana wameamua kufanya ziara katika mashina, ili kuwakumbusha viongozi wajibu wao wa kutatua kero za Watanzania.

"Hatutamvumilia mtumishi, ambaye amepewa dhamana na serikali halafu anafanya vile anavyotaka, chama hakitamvumilia ndiyo maana tumekuja kuwasikiliza na kuwauliza viongozi wana mipango gani?,"Anasema Shaka.

Anahoji:"Nimepewa taarifa hapa kuna mama kajinyima kanunua jokofu lake, leo limekufa kwa kukatika umeme mara kwa mara hapa tunawasaidia wananchi au tunawarudisha nyuma?"

## AMVAA WAZIRI MUBASHARA

Shaka anampigia simu Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato na kuweka kipaza sauti, ili wamsikie na kumuuliza ni lini atatatua tatizo hilo la kukatika umeme katika wilaya hiyo na maeneo mengine?

Byabato anasema wanaendelea kusimamia na kutekeleza, yale ambayo wameyaahidi kwenye ilani ya CCM na kwamba walikuwa na kikao cha kufuatilia kwa nini hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara.

"Maeneo mengi ni miundombinu kuchakaa na kurekebisha miundombinu hiyo. Wamekuwa hawatoi taarifa, ninakuomba kiongozi jambo hilo tumekubalina kufanya vikao vya ndani kutafuta suluhu," anasema Byabato.

Baada ya kutoa maelezo hayo, Shaka anasema chama hakipendi kuwatembelea wananchi na kusikia vilio vyao na wakiangalia kwa kiasi kikubwa badala ya kusonga mbele wanarudi nyuma.

## WAHUJUMU BANDARI KUKIONA

Shaka anawaahidi wana Mtwara kuwa watachukua hatua kali kwa wahujumu bandari ya Mtwara, ambayo imegharimu Sh bilioni 157.8, lakini utendaji kazi wake unasuasua.

Shaka anatangaza hayo baada ya kutembelea bandari hiyo akisema hawakutegemea kama mradi huo ungekwama na kuahidi hatua kali zitachukuliwa kabla ya Oktoba mosi, mwaka huu, dhidi ya wanaofanya hujuma hizo.

Mbunge wa jimbo la Mtwara mjini (CCM), Hassan Mtenga, anasema bandari hiyo inakabiliwa na changamoto ya baadhi ya watu kuihujumu, ili ishindwe kufanya vizuri kama ilivyokusudiwa.

Anasema inaweza ikafika Oktoba hujaona meli wala kontena, kutokana na hujuma zinazofanywa na baadhi ya watumishi wa serikali waliorubuniwa, ili kukwamisha bandari hiyo.

"Wapo watu hawataki kuona bandari ya Mtwara ikifanya vizuri... kwa sababu kilio kikubwa cha wananchi ni kuwa zaidi ya watu 6,000 walikuwa wanatumia bandari hiyo, hawaonekani na sasa wafanyakazi wamepoteza ajira,"anasema.

Mtenga anasema alifika Wizara ya Uchukuzi na Ujenzi na kutoa malalamiko ya kuhujumiwa bandari hiyo, lakini baadhi ya viongozi wakuu walimtaka aachane na suala hilo, jambo ambalo lilimshangaza.

"Nikajua ule mtandao bado upo nikaja na hoja nyingine, hatimaye Rais Samia Suluhu Hassan akamuagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ninamshukuru kwa hili kwa kuwa lilitolewa tamko,"anahoji mbunge.

Anasema kwa sasa wanafanya kila njia kukutana na mawaziri, ili kukwamua bandari hiyo iliyojengwa kwa gharama kubwa na kwa kutumia fedha za umma.

"Hoja yao ni makontena, lakini wenyewe wanaagiza magari nchini Japan nani anawapa kontena? Haiwezekani mtu anaagiza korosho tani zaidi ya 300,000 tena kutoka Vietnam, halafu anashindwa kuleta meli yenye kontena, nini wanachokifanya?" anahoji mbunge.

Anasema vita inazidi kuwa kubwa kwa sababu wanaopinga matumizi ya bandari wana malori ya kusafirisha korosho, kuzipeleka Dar es Salaam na wapo tayari kufanya lolote kwa baadhi ya viongozi, ili kutekeleza jambo lao.

Mbunge huyo anamuomba Shaka aende kuzungumza na Rais Samia na Katibu Mkuu wa

INAENDELEA UK.12




Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika. **PICHA: MTANDAO**

# Watanzania tatizo si utawala bora, shida kubwa ni uchumi

**Na Nimi Mweta**

KWA Afrika na Tanzania imekuwa ni jambo la kawaida, badala ya nchi kusonga mbele baada ya hatua fulani, iwe ni kupata uhuru, mfano Zimbabwe au Msumbiji, utawala wa walio wengi Afrika Kusini, kinachofuata kimekuwa ni kuharibika.

Kinachotokea kwenye mataifa mengi baada ya mafanikio badala ya kuwa chema zaidi ni kuharibika au kunakuwa na mchanganyiko wa uharibifu na uthabiti wa demokrasia kama Zambia, DRC na Tanzania pia.

Fikra inayotawala harakati za kisiasa katika Afrika ilianza miaka ya awali ya 1980, ikisukumwa na haki za binadamu na demokrasia, kama hitaji la msingi la makundi yanayokandamizwa katika mifumo tofauti. Mara nyingi ni makundi ya kitabaka kwa mfano rungu, dhidi ya waandishi wa habari na kukandamiza uhuru wa kutoa maoni.

Haya yanatokea karibu nchi zote za Afrika na mara nyingine, matatizo mengine ni ya kijamii, kunapokuwapo migawanyiko ya kina, ndani ya utaifa husika.

Dhana hii haikuingia katika suala la urekebishaji uchumi, ambalo lilijikita katika kuondoa rushwa, ufisadi, matumizi mabaya fedha za umma na kukwamisha miradi ya maendeleo.

Kukua kwa dhana hii kuliendana na mazingira ya mashindano ya kiitikadi kimatafa, wakati ujamaa wa nchi za Mashariki na ubepari nchi za Magharibi ukishindana, au wakati ubeberu ulikuwa unajihami na ujamaa unaojaribu kujitanua kwa njia za kijeshi au kimapinduzi.

Kwa vile nchi za Afrika bado zilikuwa katika hisia ya kina, kuhusu ukoloni na wasomi wake wakiwafuata wanaharakati wa Magharibi na propaganda, kutoka nchi za Mashariki waliwaaminisha watu kuwa umaskini unatokana na kudhulumiliwa na kunyonywa na nchi tajiri.

Ambacho wasomi wa Afrika na Tanzania hawakuwahi kuelewa hata wakiambiwa wanakataa, kutokana na hisia za msingi za uzalendo ni kuoanisha mifumo ya uchumi na fikra au hulka za kisiasa.

Msomi anayetaka haki za binadamu ziheshimiwe, hasa za kujieleza au kuunganisha katika vikundi na jumuiya za kiraia au za kisiasa kufuatilia dhana au madai ya pamoja, anatakiwa pia akubali uhuru wa mtu binafsi katika uchumi.

Aidha akubali pia kuwa, kuweka mifumo ya uchumi inayolenga kumwezesha mtu binafsi kujitanua kiuchumi, hivyo mawazo binafsi kupata nafasi.

Wasomi wa Afrika hawana ubaya na uchumi hodhi ukisimamiwa na dola, ila kuwe na uhuru jambo, ambalo linahitaji tafakari mpya.

Wasichokielewa ni kuwa uchumi hodhi wa dola unazuia kukua kwa sekta tofauti za uchumi kwa kasi inayohitajiwa, kukidhi idadi ya vijana, wasomi wanaotafuta ajira.

Halafu wale wanaoajiriwa katika taasisi za uchumi na utawala wanachelea kuondoka madarakani kwa kiongozi aliyepo, aje ambaye hawamfahamu au ana watu wake wenye utiii kwake, wafagiliwe wote waingie wengine. Ndiyo maana hili la kukabidhi mamlaka ya utawala kwa amani ni vigumu kwa nchi nyingi - kikionekana kama kiama kwa tabaka la watawala.

Kinachotakiwa siyo kuendelea kuhubiri katiba mpya na uwapo wa tume huru za uchaguzi, mgombea huru au kwenda mahakamani kupinga matokeo kwani hata hali hiyo ingefikiwa, siyo lazima iheshimiwe na kufikiwa kwake kunahitaji mazingira stahili katika uchumi.

Viongozi waone aibu kukataa kuondoka madarakani, huenda kinachowafanya kukataa kuondoka ni taharuki ya kinachofuata - kama kinagusa watawala wengi, basi hakitawezekana na lazima utawala uliopo utaendelea.

Ina maana kuwa wasomi Afrika na Tanzania wanatakiwa wapiganie kwanza uchumi huru, ambao dola haliusimamii.

Mwelekeo huo hautawezekana, bila wasomi Afrika kujikwamua na dhana za asili za kibaguzi zilizopo katika uzalendo wao, kwa mfano chuki ya wageni kama Waarabu, Wazungu, mfano Afrika Kusini au Zimbabwe. Nchini Kenya imeanza 'Mau Mau' nyingine katikati ya nchi, eneo la Laikipia, ambako wageni wana mashamba makubwa ya kibiashara, mfano maua, wanavamia kwa bunduki kuwaua, ili maeneo hayo yawe ya malisho kwa wafugaji wanaohamahama.

Kwa Tanzania hayo yalijitokeza Arumeru Arusha, mashamba yalifyekwa na baadhi kuuawa na wenyeji wakiyataka maeneo hayo. Ndiyo agenda ya sasa, bila kugawa ardhi kwa kila aliyepo kama milki binafsi, huwezi kuzuia wawindaji kuungana na kumiliki kinguvu.

# Ziara ya Chongolo, timu yake inavyowabana mubashara viongozi wanaolalamikiwa

**INAENDELEA UK.11**

CCM, Daniel Chongolo kuhusiana na hujuma, zinazofanywa katika bandari na kusababisha kuendelea kudorora.

"Matajiri wanatuchezea, hakuna anayeweza kuzungumzia jambo hili, wengi wao wanaogopa, ila baadhi ya wafanyabiashara wanatuchezea katika hii bandari," anasema Mtenga.

Baada ya kusikiliza maelezo hayo, Shaka anasema wamekuwa wakijiuliza maswali mengi, kwa nini mradi unakwama licha ya uwekezaji huo kuwa mkubwa na uliolenga kupunguza wimbi la umaskini na kipato kwa wananchi?

"Hatukutegemea kama mradi ungekwenda kwa kusuasua hata kama nisingepangiwa kufika bandari ni lazima ningefika, ili nijue shida ni nini mbona mambo hayaendi?".

Shaka anasema tayari Rais Samia alishatoa maelekezo na wanataka kumjua huyo, ambaye anakwamisha bandari hiyo na CCM haitamvumilia anayerudisha nyuma jitihada za Rais.

Anawapa maelekezo kuwa kabla ya Oktoba mosi mwaka huu, mamlaka zote zinazohusika zikutane, ili kujua nini kinachosababisha bandari hiyo kusuasua.

"Kama kuna watu ama genge la watu linafikiria kumkwamisha Rais Samia, chama kipo macho na imara, hii fedha iliyotumika katika mradi huu ni kubwa aliyehusika kuhujumu chama kitatoa maelekezo,"anaahidi Shaka.

**MADIWANI WAKUMBUSHWA**

Shaka anatoa agizo kwa madiwani kushuka ngazi ya chini, kwa ajili ya kutatua changamoto za wananchi na kuwaelimisha masuala mbalimbali ya maendeleo ya miradi, badala ya kukaa kimya.

Anatoa maagizo hayo akiwa katika Kata ya Mletele, Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma, wakati akiendelea na ziara yake na kutaka kila diwani kusimamia miradi ya kata yake na kutatua kero za wananchi.

Anasema hayo baada ya wananchi wa Mletele kumlalamikia Diwani wao, Maurus Lungu, kuwa hana ushirikiano na hawapewi taarifa za maendeleo ya miradi yao.

Shaka anamwita Lungu kujibu tuhuma hizo, lakini akakanusha kuwa si za kweli na mpaka sasa amefanya vikao vinne na taarifa amekuwa akiwapatia wananchi hao, ingawa hawajitokezi.

Anasema anapokuwa anafuatilia jambo likiwa limefika kwenye ngazi ya juu na kucheleweshwa wananchi hao, wanadhani anawakwamisha, lakini akasisitiza kuwa madai yao si ya kweli.

Baada ya maelezo hayo, Shaka anaahidi kuwa CCM, haitamvumilia diwani, ambaye hatimizi wajibu wake kwa wananchi ipasavyo kwa kuwa serikali inataka kila diwani kufanya kazi kuendana na kasi ya Rais Samia.

KISHINDO CHA RAIS ALIPOTUA NEW YORK

# Apagawishwa na wanadayaspora walivyofurika kumlaki uwanjani

## • Mchambuzi azitetea ni ziara zenye tija



Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kuwasili jijini New York, Marekani. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

"TUNA imani na Samia, oyaa oyaa oyaa...maama mama, mama huyo, mama, yetu eeh, mama huyo mama'. "

Hivyo ni vibwagizo na bashasha zilizosikika kutoka kwa baadhi ya wanadayaspora ya Tanzania walioko Marekani, walipojitokeza kumpokea Rais Samia Suluhu Hassan, anayezuru nchi hiyo.

Rais Samia, ametinga jijini New York Jumapili iliyopita kuhudhuria mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA), ambapo pia anapokelewa na Watanzania hao na kuwashukuru kwa mapokezi makubwa.

Ni mara ya kwanza Rais Samia kushiriki katika mkutano huo wa UNGA kama kiongozi wa nchi, huku Tanzania ikiwa imeshawasilisha ripoti ya kuonyesha jinsi ilivyotekeleza vipaumbele vyake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs ).

Ikihojiwa na Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa, Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Kimataifa, Balozi Liberata Mulamula, anasema, Tanzania imejipanga kwa mikakati inayogusa malengo yote 17 ya SDGs.

Akigusia nafasi ya mwanamke, Balozi Mulamula anasema, Tanzania ina Rais mwanamke, na kwamba mapinduzi hayo bado yanaendelea ili kuhakikisha wanawake na vijana wengi zaidi wenyye vigezo wanapata nafasi za uongozi.

"Tanzania kuwa na mama katika nafasi ya urais, ni ni kwamba, mapinduzi yanakuja, kwani hata kwenye uteuzi wa nafasi mbalimbali, wanawake wamepewa kipaumbele hasa wale wenye sifa," Balozi Mulamula anasema.

Kwa sasa itatajwa kuwa mataifa yenye viongozi wanawake kama ilivyokuwa Kwan Malawi na Liberia.

Rais mwanamke, Afrika Mashariki ilianzia Burundi wakati Sylvia Kinigi ambaye alianzia kwenye nafasi ya Waziri Mkuu wa nchi hiyo mwaka 1993, lakini mwaka huo huo hadi 1994, akawa Kaimu Rais wa Jamhuri ya Burundi.

Alikuwa Kaimu Rais wa Jamhuri ya Burundi baada ya aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Melchior Ndadaye kuuawa kwenye vita ya yenyewe kwa wenyewe ambapo alifanikiwa kuwakusanya mawaziri 15 kati ya 22 na kuongoza nchi hiyo ikiwa katika mgogoro mkubwa wa kisiasa.

> "Lakini kipekee Rais anatekeleza lengo la kuongeza kasi ya ushirikiano na mtangamano wa kisiasa, kijamii na kiuchumi kikanda kama sera inavyosema.

Wanawake wengine marais ni Joyce Banda aliyekuwa Rais wa Malawi kuanzia 2012 hadi 2014 na Ellen Johnson Sirleaf aliyeiongoza Liberia kuanzia mwaka 2006.

Hao ni baadhi ya marais wanawake waliowahi kuongoza nchi, lakini pia wapo ambao hadi sasa wako madarakani, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan na Sahle-Work Zewde wa Ethiopia.

**ZIARA ZA RAIS NG'AMBO**

Mchambuzi wa siasa na Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia Dar es Salaam, Abbas Mwalimu anasema, marais wana aina nne au tano za safari, kuanzia ziara rasmi ya kitaifa (state visit) na za kiofisi (official visit).

"Ziara nyingine ni za kikazi na za kiofisi japo zipo za kibinafsi , ambazo hufanyika kutokana na mwaliko wa kiongozi wa nchi moja kumualika mwenzake kwenda nchini mwake," anasema Mwalimu.

Anatolea mfano wa ziara ya aina hiyo kama ile ya Rais Samia alipoalikwa na Rais Uhuru Kenyetta wa Kenya kwa ziara rasmi nchini humo, na kwamba ziara kama hiyo amewahi kuifanya Rwanda na pia Burundi.

"Ziara hii huambatana na kupigiwa mizinga 21, kukagua gwaride rasmi, kupewa zawadi, kuhutubia taifa na dhifa ya kitaifa kufanyika ikulu ya nchi husika. Inafaa kujiuliza, je Rais angekataa mwaliko?

Mchambuzi huyo anasema, Rais ana jukumu la kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje na kwamba kama anakataa mwaliko, anakuwa anaakinzana na sera ya Tanzania iwapo haendi katika ziara.

"Katika pitapita zangu nilikutana na watu wakijadili safari za Rais ikiwamo ya Marekani, ili kujenga uelewa wa pamoja juu ya safari hizo, nimeona nitoe ufafanuzi kuhusu aina tano za safari za viongozi kama marais au mawaziri wakuu kwa nchi za kifalme," anasema.

**SERA YA TANZANIA**

Anasema, sera ya Tanzania ya mambo ya nje inaelekeza utekelezaji wa misingi ya sera ya asili iliyotolewa kwa Waraka Namba 2 wa mwaka 1964.

"Imebainisha kuimarisha ujirani mwema kwa kusema. Hatuoni kuwa asipotekeleza wajibu huu wa kuimarisha ujirani mwema atakuwa amekiuka katiba? Anahoji mwanazuoni huyo.

Kuhusu ziara ya kiofisi, anasema, Rais huifanya ili kuhudhuria vikao vya taasisi na jumuiya za kimataifa, akitolea mfano kuwa, kati ya Agosti 17 na 18 mwaka huu, alikwenda Malawi kuhudhuria kikao cha 41 cha Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

"Vikao hivi ni vya lazima kwa mujibu wa itifaki iliyoanzisha umoja huu ya mwaka 1993. Vikao hivi ni kama vya Umoja wa Afrika (AU), hivyo kuhudhuria kwake ni sehemu ya majukumu ya Rais ya Kiofisi ndiyo maana safari zake huitwa ziara ya kiofisi," anasema.

Katika mwendelezo wa ufafanuzi wake anasema, kuhudhuria kwa Rais katika vikao vya SADC na AU ni kanuni iliyopo katika Sera ya Tanzania ya Mambo ya Nje inayoelekeza uimarishaji wa umoja wa Afrika.

"Lakini kipekee Rais anatekeleza lengo la kuongeza kasi ya ushirikiano na mtangamano wa kisiasa, kijamii na kiuchumi kikanda kama sera inavyosema.

Anasema, kinachofanywa na Rais Samia ndiyo uhalisia wa uhusiano wa kimataifa ulivyo, na kuongeza kuwa uhusiano huo una kanuni na kwamba marais waliomualika Rais wataalikwa kuzuru Tanzania.

"Kwa mantiki hiyo, hakuna ubaya wowote kwa Rais kusafiri pale anapoalikwa na Rais mwenzake, au anapokwenda kwenye mikutano kama huu wa Umoja wa Mataifa ama anapokwenda kushuhudia utiaji saini wa makubaliano katika nchi ya jirani kama tuna mkataba nayo kwenye jambo fulani. Ndivyo uhalisia wa uhusiano wa kimataifa ulivyo," anasema.

## VLADIMIR PUTIN

# Miongo miwili madarakani, ataishi ikulu hadi 2036

## ■Ni shujaa kuwabinya wapinzani, japo anachukiwa kashinda tena



Rais Vladimir Putin, amebadilisha katiba, ambayo inamwezesha kukaa madarakani hadi 2036. **PICHA MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Vladimir Putin wa Russia, amekuwa madarakani kwa miaka 20, akiongoza taifa hilo kama Rais, ambaye pia aliwahi kutoka ikulu na kushika wadhifa wa uwaziri mkuu.

Kiongozi huyo ni jasusi mbobezi aliyefanya kazi na Shirika la Ujasusi la Russia KGB, pia amewahi kuwa Naibu Meya wa Moscow. Putin amepaa na kuwa mtawala wa kudumu wa Russia, akimrithi Boris Yeltsin, baada ya kujiuzulu mwaka 1999.

Miaka ya mwanzoni ya 2000, Putin alipoingia ikulu maarufu Kremlin, alitaka kuwa karibu na mahasimu wake, ambao ni mataifa ya magharibi na kueleza nia ya kujiunga na Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi (NATO), lakini baadaye akabadilisha mawazo na kuachana na mpango huo.

Rais wa Russia, kwanza anakuwa Rais, kisha Waziri Mkuu na baadaye kuwa Rais aliyebadilisha katiba, ili aendelee kuishi Kremlin, akiwa sasa amefanikiwa kutimiza lengo hilo, akidumu miaka 20 madarakani.

Anawapuuza wanaomkosoa akisema hiyo ni demokrasia ya Russia, japo wakosoaji wake wanamuona dikteta anayeng'ang'ania madarakani .

Mwaka 2018, alipata ushindi wa kumbakiza tena madarakani miaka mingine sita, kabla ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika 2024.

Katika kuendeleza hatima yake ya kuishi Kremlin, wiki iliyopita, Russia ilipiga kura na Chama Cha United Russia cha Rais Vladimir Putin, kikaibuka kidedea kwenye uchaguzi wa wabunge na sasa anasherehekea ushindi wa kuwa na idadi kubwa ya wabunge kwenye Duma au Bunge la Russia.

Kura zote zikiwa zimeshahesabiwa Puttin anajizolea asilimia 50 ya kura licha ya kuonekana kuwa ushindi umeshuka kiasi, ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Katika uchaguzi huo,Tume ya Uchaguzi ya Russia inapinga kwangu zote kuwapo na vitendo vya unyanyasaji kwa wapigakura.

> “Ikiwa United Russia itashinda, nchi yetu inaweza kutarajia miaka mingine mitano ya umaskini, ukandamizaji na mingine mitano itakayopotea,” unasema ujumbe wa mpinzani mkuu wa Putin, Alexei Navalny aliye kizuizini kwa wafuasi wake.

Matokeo yanaonyesha kuwa Chama Cha Kikomunisti, ambacho ni mpinzani wa United Russia kinachoongozwa na Puttin kilikuwa na asilimia 19 ya kura.

Kwa ushindi huo chama tawala kitakuwa na zaidi ya theluthi mbili za wabunge 450 wa chombo hicho cha kutunga sheria -Duma.

Russia wamepiga kura siku tatu kuanzia Ijumaa hadi Jumapili ikiwa ni siku ya mwisho ya uchaguzi wa ubunge uliofanyika kwa siku tatu katika taifa hilo lenye maeneo 11, yenye majira tafauti ya nyakati.

**KUSHINDA KIULAINI**

Chama cha Rais Vladimir Putin, United Russia, kilitazamiwa kupata ushindi mkubwa, baada ya serikali kulinyamazisha vuguvugu la Kiongozi Mkuu wa Upinzani, Alexei Navalny na kuwazuia wapinzani kushiriki uchaguzi huo.

Ushindi huo uliotarajiwa utatumiwa na ikulu ya Kremlin, kama kielelezo cha jinsi Rais Putin anavyoungwa mkono licha ya hali ngumu ya uchumi, kuendelea kuwaathiri raia wa nchi hiyo.

Chama cha United Russia kinamuunga mkono Putin, mwenye umri wa miaka 68, ambaye licha ya umashuhuri wake kushuka, bado ndiye anayefahamika zaidi miongoni mwa wapinzani wake, kwenye karatasi ya kura yenye wagombea wa Chama Cha Kikomunisti na kile cha cha Kihafidhina, LDDR, ambacho mara nyingi huunga mkono serikali.

**IKULU HADI 2036**

Kwa sasa, United Russia ina takribani robo tatu ya Bunge Kuu la Taifa, Duma, lenye viti 450.

Hiyo iliisaidia ikulu ya Kremlin kupitisha mabadiliko ya kikatiba, ambayo yanamruhusu Putin kuwania kwa miongo mingine miwili zaidi, urais baada ya mwaka 2021, ikimaanisha kuwa anaweza kusalia madarakani hadi mwaka 2036.

“Ikiwa United Russia itashinda, nchi yetu inaweza kutarajia miaka mingine mitano ya umaskini, ukandamizaji na mingine mitano itakayopotea,” unasema ujumbe wa mpinzani mkuu wa Putin, Alexei Navalny aliye kizuizini kwa wafuasi wake.

Tume ya Uchaguzi ya Urusi, inasema asilimia 99 za kura zilizohesabiwa chama cha Puttin kimejizolea asilimia takribani 50 ya kura, wakati mpinzani wake anayeunga mkono serikali Communist Party, akijipatia takribani asilimia 19 na LDPR ikipata asilimia tisa.

**MAANA YA UCHAGUZI**

Unatafsiriwa kuwa ni kutimiza azma ya Putin kuendelea kubaki madarakani na kujipatia ushindi wa mwaka 2024, kwenye uchaguzi wa urais.

Uchaguzi wa Russia umeshuhudia wapinzani wa Puttin na wakereketwa, watetezi wa haki za binadamu wakifungiwa magerezani na kukatazwa kushiriki mchakato huo.

Tomila Lankina, Profesa wa Mahusiano ya Kimataifa katika Shule Kuu ya Uchumi ya London School of Economics, anasema uchaguzi huu umethibitisha kwa hali ya juu udanganyifu, vitisho vya dola na vipigo, dhidi ya waangalizi wa uchaguzi.

Umekosa upinzani wa kweli baada ya serikali kukataza vyama vyenye ushirikiano na Alexey Navalny, mpinzani mkuu wa Puttin kukaaa kando.

**MBINU CHAFU WAPINZANI**

Washirika wa Navalny walizuiliwa kuwania ubunge baada ya vuguvugu lake, kupigwa marufuku Juni mwaka huu, kwa madai ya kuwa ni kundi la siasa kali. Viongozi wengine wa upinzani wanadai kuandamwa kwa mbinu za kampeni chafu.

Mfanyabiashara mkubwa kutoka Chama Cha Kikomunsti anasema alizuiwa kuwania nafasi kinyume na sheria, huku mgombea mmoja wa Chama cha kiliberali katika mji wa St. Petersburg akisema majina mawili yanayofanana na yake yaliwekwa, ili kuwababaisha wapigakura.

Lakini ikulu ya Kremlin inakanusha ukandamizaji unaofanywa kwa nia za kisiasa na badala yake inasema watu wanahukumiwa kwa mujibu wa sheria walizozivunja. Ikulu hiyo na chama cha United Russia inakanusha kuhusika na mchakato wa kuwasajili wagombea.

Kambi ya Navalny ilitumia mbinu ya kumshinda Rais Putin kwa kuwataka wapiga kura kuwachagua wagombea walioonyesha upinzani mkali kwa wale wa United Russia, lakini mamlaka nchini Urusi, zimekuwa zikijaribu kuzuwia kampeni hiyo kufanikiwa.

“Siku moja, tutaishi Russia itakayowezekana kuwapigia kura wagombea wazuri, walio kwenye majukwaa tafauti ya kisiasa,” anasema mshirika wa Navalny, Leonid Volkov, kwenye ujumbe wa mtandao wa Telegram





# Miradi 115 iliyokwama yaanza kutoa maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa miradi ya maji 115 kati ya 177 iliyobainika kuwa ya kichefuchefu imefanyiwa marekebisho na imeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari na wahariri jijini hapa, Mkurugenzi wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira kutoka Wakala wa Majisafi na Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkama Bwire, alisema hadi kufikia Juni mwaka huu miradi hiyo imekamilika, huku iliyobaki 62 inatarajiwa kurekebishwa ifikapo Desemba 2021.

"Tulipokea miradi 632 iliyokuwa inatekelezwa na Halmashauri ya Wilaya na hadi kufikia mwaka huu miradi 566 imekamilika na inatoa huduma kwa wananchi, wakati tunapokea kulikuwa na miradi 177 ilikuwa na changamoto ya kutotoa huduma kwa wananchi lakini hadi Juni mwaka 155 imekamilika, na 62 bado tunaendelea nayo," alisema.

Alibainisha kuwa kukamilika kwa miradi hiyo kumesaidia kuongeza hali ya upatikanaji maji vijijini.

Alifafanua kuwa Wakala huo wakati unaanza kutoa huduma mwaka 2019, hali ya upatikanaji maji vijijini ilikuwa asilimia 64.7 hadi kufikia Juni mwaka huu ni asilimia 72.3 huku malengo ni kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

Bwire alisema katika bajeti ya mwaka 2021/22, Wakala huo umetengewa bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni 450 na inatarajia kutekeleza mikataba 1,176 ya miradi ya maji.

"Katika kuongeza kasi ya utekelezaji mikataba tumeigawa katika makundi mawili ambapo tunatarajia miradi mingi itatekelezwa kupitia makandarasi na tumepanga mikataba 779 itatekelezwa na makandarasi na tayari tumeshawatambua makandarasi wenye sifa tutakaowatumia kutekeleza miradi," alisema.

Alisema mikataba ya miradi 397 itatekelezwa na wataalamu wa ndani ambapo kukamilika kwake kutaongeza upatikanaji wa maji kwa asilimia 3.7.

"Tunaamini katika kutumia nguvu ya wakandarasi miradi mingi itakamilika mwaka huu na kuongeza hali ya upatikanaji maji kwa wastani wa asilimia 3.7 mwakani na hivyo tutakuwa tumesogea kufikia asilimia 77 kuelekea safari yetu ya kufikia asilimia 85," alisema.

Kuhusu utafutaji wa vyanzo, Mkurugenzi huyo alisema mwaka huu wamepanga kuchimba visima 516 kati ya hivyo 250 vitachimbwa na sekta binafsi na vingine watatumia Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa nchini (DDCA).

"Pia katika utafutaji wa vyanzo kuna ujenzi wa mabwawa ambapo kwenye eneo hili tumejipanga ambapo kuna mabwawa 15 tunataka tukamilishe mwaka huu wa fedha na mengine yanaendelea kujengwa na mengine tutaanza kujenga mwaka huu wa fedha, ili kila wilaya iwe na bwawa ili kutatua tatizo la maji," alisema.



Wakazi wa Jiji la Dodoma, wakisafisha matairi chakavu, eneo la Nyerere Square jijini humo jana, kwa ajili ya kuyauza ili wajipatie riziki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TWPG: Vijana komesheni ukatili wa kijinsia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Wabunge Wanawake (TWPG), Shally Raymond, amewataka vijana kushiriki kikamilifu kukomesha vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

Pia, amewataka wanawake vijana kujitokeza kwa wingi kushiriki uchaguzi mkuu 2025, ili wafanikishe kumuweka madarakani Rais mwanamke.

Shally, alitoa wito huo wakati akifunga mafunzo yaliyowakutanisha wanawake vijana 30, yaliyoandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kushirikiana na kituo cha usuluhishi (CRC) pamoja na Young and Alive Initiative na shirika la Mawasiliano Afrika (Femnet). Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku nne, jijini hapa yakiangazia masuala ya uongozi na nafasi ya mwanamke katika siasa.

Mwenyekiti huyo ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (CCM), alisema ni vyema vijana wanapotaka kuwa viongozi wakajifunza kwa waliowatangulia.

"Ukiwa kiongozi halafu ukawa mchoyo kwa kuwaelimisha wenzio kuhusu masuala ya uongozi wakati wewe pia ulifanikiwa kwa kujifunza kutoka kwa waliotangulia na kufanikiwa, kamwe hautofika mbali,"alisisitiza.

Kuhusu ukatili na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vilivyopo katika jamii, alisema kila mmoja ana

jukumu la kuhakikisha vitendo hivyo vinakoma hususani dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema wao kama wanawake vijana wanaojiandaa kuwa viongozi wa kesho, lazima wayajue masuala hayo na kushiriki kikamilifu kuyatokomeza.

"Hakikisheni mnakuwa wawajibikaji, pamoja na kuwajibika kwenye majukumu yenu ya kazi na familia pamoja na kulinda haki zenu, pia msimamie na masuala hayo maana sifa ya mwanamke ni kutochoka licha ya kuwa na majukumu mengi," alisema.

Alisema maandalizi ya uchaguzi mkuu mwaka 2025, yanapaswa kuanza mapema, hivyo wanawake lazima wajipange ili waweze kumuweka rais mwanamke madarakani itakapofika muda huo.

"2025 wanawake tunajambo letu hivyo tujipange na muda ukifika tujitokeze kwa wingi," alisema.

Akizungumza kuhusu ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Godfrey Sansa, alisema baadhi ya watu wanadhani ushiriki wa wanawake ni lazima uwe wa siasa, lakini ipo haja ya wanawake kuwa washiriki wa mabadiliko kuanzia ngazi ya jamii.

Alisema haki ya mwanamke inaweza kulindwa endapo atakua sehemu ya mchakato wa haki hizo.

Mwanasheria kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Fausta Mahenge, alisema bado mwamko wa wanawake kushiriki kugombea nafasi za uongozi uko chini huku akiwataka kutekeleza masharti pindi wanapoteuliwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

# Kada wa BAWACHA aunga mkono juhudi, sasa ajiunga na CCM

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) Mkoa wa Dodoma, Eva Mpagama, amejiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa madai kuwa ameridhishwa na utendaji kazi wa miradi mikubwa iliyoachwa na Hayati John Magufuli.

Akizungumza juzi baada ya kukabidhi kadi ya CHADEMA kwa Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Mbaga, alisema kuwa amejiunga na CCM kutokana na kuridhishwa na utendaji kazi wa iliyokuwa serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati Magufuli.

Alisema pia amevutiwa na utendaji wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo anatekeleza miradi mingi ambayo mpaka sasa inaendelea kukamilika.

"Nisiwe muongo nimekuja CCM sababu ya Magufuli, ameitendea haki nchi hii kila sehemu kumetifuliwa kuna ujenzi unaendelea...nimekaa nimejitafakari nimeona nije CCM kuendeleza yake mazuri ambayo yamefanya na nina imani Rais wa sasa anaendelea kuyatekeleza yale mazuri ambayo yamefanywa,"alidai.

Mpagama, alisema kuwa sasa anajipanga kuendelea kukipigania Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha yale mazuri ambayo yanaendelea kufanywa anawajibika ipasavyo kama ilani ya chama inavyotaka kuwa kila mmoja aweze kufahamu wajibu wake.

Kwa upande wake, Katibu wa CCM, Mkoa wa Dodoma, Pili Mbaga, alimpongeza Eva kwa kujiunga na CCM ambapo amedai uamuzi aliofanya ni mzuri na hata hivyo alionekana kuchelewa kuungana na CCM.

"Huku ndio kila kitu, sisi tunakukaribisha kwa mikono miwili kama CCM Mkoa, lakini unatakiwa uende kwenye eneo lako shina ili uweze kupatiwa kadi ya uanachama, CCM Mkoa wa Dodoma itaendelea kuhakikisha inaendelea kumuunga mkono Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya," alisema.

# RC aagiza utengenezaji mipango miji haraka

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, ameagiza wakurugenzi wa halmashauri wakishirikiana na watumishi wa ardhi, kutengeneza mipango miji haraka yenye kuzingatia uhifadhi mazingira, maeneo wazi ya watoto na kutenga maeneo ya viwanda vidogo vidogo vinavyoongeza thamani ya mazao mbalimbali yanayozalishwa kwa wingi.

Mgumba alitoa kauli hiyo juzi akizungumza na wakuu wa Idara ya Ardhi na watumishi wengine wa mkoa huo.

Alisema Mkoa wa Songwe bado haujapangwa vizuri hali inayosababisha wananchi kutozingatia uhifadhi wa misitu, maeneo ya wazi kwa ajili ya watoto kucheza, kuvamia na kujenga maeneo yenye rutuba yanayofaa kwa kilimo.

Alisema watumishi wa ardhi mkoa wakishirikiana na wakurugenzi wanatakiwa kuanza mara moja kurasimisha ardhi na kupanga miji kulingana na uhitaji wa halmashauri huku uhifadhi wa mazingira ukifuatwa ili miji iendelee kuwa ya kijani.

"Maeneo yarasimishwe na kupangwa kulingana na uhitaji wa viwanda, biashara na kilimo na ufugaji. Kuna maeneo ni mazuri kwa kilimo, lakini yamevamiwa na kuwa makazi ya watu," alisema Mgumba.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Songwe, Suma Mwakasitu, alisema mpaka sasa ni Halmashauri ya Mji Tunduma pekee ambayo tayari imepima na kupangilia mji wake.

Alisema pamoja na mkoa kuwa mpya wamejipanga kuhakikisha halmashauri zote za mkoa wa Songwe kupima na kutenga maeneo kwa ajili ya kilimo, viwanda, biashara utunzaji uhifadhi wa misitu na makazi.

"Tuna mpango kabambe kuhakikisha Mkoa wa Songwe kuwa kwenye mpangilio mzuri tukishirikiana na wakurugenzi wa halmashauri zote," alisema Mwakasitu.

Kwa upande wake, mkazi wa Vwawa, Sophia Mwashiuya, alisema kukosekana kwa mipango miji hususan katika mji wa Vwawa husababisha wananchi kushindwa kusaidiwa wanapopata majanga kama ya moto.

Alisema siku hizi watoto hawana maeneo ya michezo wanapokuwa nyumbani, jambo ambalo huchangia kupoteza vipaji vyao vya michezo kama riadha na mpira wa miguu.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (katikati), akizungumza na wananchi alipotembelea Wakala wa Taifa wa Chakula (NFRA) na kujionea zoezi la ununuzi wa nafaka za mahindi linavyoendelea, mjini Songea, mkoani Ruvuma juzi. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# Ukosefu mahakama wachangia matukio ya uhalifu

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MKUU wa Wilaya ya Songwe, Simon Simalenga, amesema kukosekana kwa mahakama ya wilaya kumechangia kuwapo kwa matukio mengi ya uvunjifu wa amani hasa ya ujambazi, uporaji na mauaji.

Akizungumza na Nipashe jana, Simalenga alisema kuwa ili kukabiliana na vitendo viovu wananchi wanapaswa kupata huduma ya mahakama karibu na maeneo yao wapate haki zao kwa mujibu wa sheria.

Alisema Wilaya ya Songwe inashughuli nyingi za kiuchumi hasa uchimbaji madini zinazochangia kukusanya watu kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi na kuibuka matukio ya ujambazi.

Alisema wilaya hiyo inapakana na mikoa ya Tabora, Rukwa na Katavi na kusababisha mwingiliano mkubwa wa watu ambao huweza kuchangia vitendo vya uhalifu hususan kwenye maeneo ya migodi na mapori ya wanyama.

"Hadi sasa wananchi wangu wanaenda kupata huduma za kimahakama katika Wilaya ya Mbozi kilomita 155 vilevile hadi kufika Gereza la Songwe ni kilomita 160 kutoka hapa hivyo tunahitaji huduma hii isogezwe karibu ili wananchi wapate haki zao," alisema Simalenga.

Naye MKuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya, alisema wilaya yake inatumia jengo la Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika shughuli za kimahakama.

Alisema Wilaya ya Ileje ina mwingiliano mkubwa na watu kutoka Malawi kwa kuwa ipo mpakani na kuomba kuboreshewa huduma hizo ili kazi ziweze kufanyika kwa ufanisi.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alisema wamebaini kuwa Mkoa wa Songwe una vikwazo vingi ambavyo vinatakiwa kufanyiwa kazi haraka.

Aliwaagiza viongozi wa Songwe kuorodhesha changamoto mbalimbali zikiwamo za ukosefu wa mahakama, miundombinu na upungufu wa watumishi na kumkabidhi Jaji Mkuu Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuzifanyia kazi ndani ya muda mfupi.

# Vijiji 82 vyaunganishiwa umeme wilayani Mbarali

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

JUMLA ya vijiji 82 kati ya 102 vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya vimeunganishwa na huduma ya nishati ya umeme, vijiji 20 vilivyobaki mchakato wa kuviunganisha umeanza.

Kwa mujibu wa Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Nicodemusi Kapange, wanaendelea na jitihada za kuhakikisha vijiji vyote 20 vilivyosalia vinapata umeme huku vitongoji navyo vikiunganishwa.

Kapange alisema wanaendelea kuhamasisha wananchi kuepuka vishoka ambao hupita majumbani wakidai ni maofisa TANESCO na kuwaunganishia umeme kwa gharama kubwa.

Alisema bei elekezi ya kuunganisha umeme ni Sh. 27,000 na kwamba tangu mtu analipia inachukua siku 30 mteja kuunganishiwa nishati hiyo.

"Tunaendelea na mchakamchaka wa kuwaunganishia wateja umeme naamini vijiji vyote 102 vitaunganishwa na huduma kikubwa wananchi kuepuka vishoka ambao hujifanya watumishi wa TANESCO huwaunganishia watu kinyemela, tunaendelea na misako wanaobainika tunawashughulikia kwa mujibu wa sheria," alisema Kapange.

Aliwashauri wananchi fedha za malipo ya kuunganishiwa umeme zilipwe katika ofisi za TANESCO na sio kumkabidhi mtumishi mtaani kwa kuwa zinaweza zisifikishwe kwenye eneo husika.

Aliongeza kuwa hadi sasa wamebadili nguzo 232 zenye urefu wa mita 12 na wamekata miti iliyo kwenye njia kuu ya umeme umbali wa kilometa 234 lengo likiwa kuhakikisha tatizo la kukatika umeme Mbarali linakuwa historia wilayani humo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alimtaka Meneja wa TANESCO kuendelea kuboresha miundombinu ya umeme ili tatizo la kukatika kwa umeme liwe la kihistoria.

Alitoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kuwatumia vishoka kuunganishiwa umeme badala yake wafike ofisi za shirika hilo kupewa wataalamu.

Kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na timu yake, amekuwa akitoa ushirikiano mkubwa na tunakoelekea tatizo la umeme litakuwa historia.

Nitoe wito kwa wananchi kubadilika, hakuna malipo ya serikali yanayofanyika mkononi malipo yote yanafanyika kwa kutumia control namba ambayo unapewa na TANESCO na kwa wale wanaofanya ujanja ujanja nawaomba wananchi wawe wanatoa taarifa mapema ili tuwashughulikie.

Katika hatua nyingine Mfune alisema serikali imetoa kiasi cha Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu za wagonjwa katika hospitali ya wilaya.

Alisema ujenzi wa wodi hizo utasaidia kukabiliana na uhaba wa vyumba vya kulazwa wagonjwa katika hospitali hiyo na kuwahakikishia wananchi kuwa wataendelea kupata huduma bora za matibabu.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila aliwasisitiza wananchi kuchukua dhidi ya ugonjwa wa corona na kuwahamasisha kufuata taratibu zote za afya zilizotelewa na viongozi wakuu wa nchi pamoja na Wizara ya Afya zikiwamo kuvaa barakoa sehemu zenye mikusanyiko, kuepuka misongamano isiyo ya lazima na kufanya mazoezi ili miili izidi kuwa imara.





# Muswada kupambana dawa za kulevya waiva

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametakiwa kujiandaa kuuchangia Muswada wa Sheria ya Dawa za Kulevya ambao utakaounda mamlaka kamili ya kupambana na wimbi la dawa hizo yenye uwezo wa kukamata, kufanya upelelezi pamoja na kufikisha mahakamani.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, wakati akijibu hoja mbalimbali za wajumbe waliochangia ripoti ya dawa za kulevya ya mwaka 2019-2020.

Alisema Sheria ya Dawa za Kulevya iliyopo sasa inaundwa na Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya ambayo kazi yake ni kusimamia mwenendo wa dawa za kulevya huku kazi kubwa ikifanywa na taasisi nyingine.

Alisema kazi ya kukamata watuhumiwa wa dawa hizo na kufanya upelelezi pamoja na kufikisha mahakamani inafanywa na Jeshi la Polisi ambalo kwa kiasi kikubwa limeibua malalamiko mengi kuhusu utekelezaji wake.

Alisema sheria iliyopo sasa imebainika kuwa na upungufu na kushindwa kutekeleza majukumu yake vizuri katika kupambana na dawa za kulevya na ndiyo maana bado lipo wimbi kubwa la dawa hizo.

"Nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tutaleta sheria mpya ya kuunda mamlaka kamili ya kupambana na dawa za kulevya ambayo itakuwa na uwezo wa kukamata watuhumiwa, kuwafikisha mahakamani pamoja na kufanya uchunguzi yenyewe," alisema.


Alisema katika kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya serikali inakusudia kuimarisha polisi jamii ambayo itafanya kazi ya kusaidia kazi za kufuatilia athari hizo.

Alisema dawa za kulevya zipo katika jamii na wananchi wanawafahamu watu wanaofanya biashara hiyo katika shehia zao.

"Tutapounda mamlaka kamili ya kupambana na dawa za kulevya tutaimarisha polisi jamii ambayo itasaidia mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika ngazi za shehia ambapo biashara hiyo inafanyika," alisema.

Alisema katika kuundwa kwa mamlaka kamili ya kupambana na dawa za kulevya baadhi ya taasisi zitaimarishwa ikiwamo kitengo cha Mkemia Mkuu wa Serikali ambacho miongoni mwa majukumu yake ni kufanya uchunguzi na kutoa taarifa ya madawa ya kulevya yaliyokamatwa kujua uhalisia wake.

"Zipo baadhi ya dawa za kulevya zimelazimika kutelekezwa au wahusika wake kuachiwa huru baada ya taarifa ya uchunguzi kuonyesha kwamba sio dawa halali," alisema.




Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Lela Muhammed Mussa, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Kituo kuzalisha vifaranga vya samaki, majongoo chaanza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Abdalla Hussein Kombo, amesema kwamba tayari kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki pamoja na majongoo ya pwani kimeanza uzalishaji na kuwataka wafugaji wa samaki kuchukua vifaranga kwa uzalishaji wa mazao ya baharini.

Kombo alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Omar Hamadi, aliyetaka kujua maendeleo ya kituo cha kutotoa vifaranga vya samaki wa baharini lini kitaanza uzalishaji wake.

Akitoa ufafanuzi huo, Kombo alisema kituo hicho ambacho kimejengwa chini ya msaada wa Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo ya Korea (KOICA), kimeanza uzalishaji wake baada ya kusita kutokana na hitilafu za kitaalamu.

Alisema vifaranga vinavyozalishwa kwa sasa ni pamoja na majongoo ya pwani, kaa na samaki aina ya kambare na mwatiko.

Aliwataka wafugaji wa vifaranga kujitokeza kuchukua mazao ya baharini kwa ajili ya kujiimarisha kiuchumi kufuatia kujitokeza kwa mahitaji.

Alisema majongoo mahitaji yake ni makubwa ambayo mfugaji yanaweza kumwinua kiuchumi na maendeleo na kuepukana na umaskini.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi wa Baharini ni kutoa elimu kuhusu ufugaji wa mazao ya baharini kwa wananchi wa makundi mbalimbali Unguja na Pemba.

"Wafugaji wa mazao ya baharini tunawataka waje katika kituo cha kutotoa vifaranga kilichoko Beit-el-Ras kuchukua vifaranga vya aina mbalimbali ambavyo tumeanza kuzalisha tena ikiwamo majongoo ya pwani, kaa pamoja na kambare," alisema.

## Wabunge watakiwa kuongeza kasi kuleta maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Job Ndugai, amewataka wabunge kuongeza kasi ya kuwaletea maendeleo wananchi katika majimbo ya uchaguzi kwa kutumia fedha za mfuko wa jimbo.

Ndugai alisema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwamo wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yeye akiwa mlezi wa chama mkoa huo.

Alisema majukumu ya viongozi wa majimbo ikiwamo wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na madiwani ni kuharakisha maendeleo kwa kuongeza ubunifu wa miradi kwa kushirikiana na viongozi wa jimbo.

Alisema wananchi wamejenga matumaini makubwa kwa viongozi waliowachagua wa majimbo ya uchaguzi katika kuharakisha kuleta maendeleo katika miradi mbalimbali itakayowainua kiuchumi.

"Kazi yetu kubwa sisi viongozi wa majimbo ya uchaguzi ni kuhamasisha maendeleo na kubuni miradi itakayowainua kiuchumi na kupambana na umaskini," alisema.

Ndugai amefurahishwa na kasi ya kuleta maendeleo ya mawasiliano na usafirishaji kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja baada ya kutembelea miradi mikubwa ikiwamo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigunda uliopo Nungwi pamoja na ujenzi wa Bandari ya Mkokotoni Unguja.

Alisema kuwapo kwa miradi hiyo kwa kiasi kikubwa itasaidia kuongeza mapato ya kiuchumi kwa serikali kuu ikiwamo kuimarika kwa huduma za usafirishaji na kupokea mizigo katika bandari hiyo kutoka mikoa jirani ya Tanzania Bara.

"Miradi hii ni muhimu ambayo itasaidia kuimarisha huduma za wananchi kiuchumi pamoja na serikali kuingiza mapato na kukua kwa sekta ya utalii," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema wabunge wa mkoa huo wana ushirikiano mzuri wa kasi ya kuleta maendeleo na kusimamia miradi ya ujenzi wa shule, vituo vya afya na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

"Mheshimiwa weye ni mlezi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kichama hapa tunafanya kazi vizuri na kushirikiana na wabunge na viongozi wengine katika kuwatumikia wananchi na kutekeleza miradi ya maendeleo ya ujenzi wa shule na hospitali," alisema.

Baadhi ya wabunge wa majimbo ya Mkoa wa Kaskazini Unguja, wamefurahishwa na ziara hiyo huku wakiahidi kufanya kazi karibu na wananchi kusimamia miradi ya maendeleo na kuzitumia vizuri fedha za miradi ya jimbo.

Mbunge wa Jimbo la Bumbwini, Mbarouk Khatib, alisema wabunge wamejipanga kuhakikisha changamoto zote ziliopo katika maeneo zinafanyiwa kazi ikiwamo miradi ya maendeleo ya kijamii.

"Miradi yote ya ujenzi wa shule na hospitali na usambazaji wa majisafi na salama pamoja na kuvisaidia vikundi vya kinamama inashughulikiwa vizuri kuona utekelezaji wa ilani na ahadi zetu wakati wa kuomba kura tunatekeleza," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

PATA MKOPO WA HARAKA KWA
MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES
FINANCE LIMITED (EFL).
KWA MAWASILIANO ZAIDI
**TUPIGIE:0677 111 333**
**AU 0758 112 332**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



**NEEMA MASHALA GOGADI** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuavyo:

1. Cheti cha **Bachelor Degree in Human Resource Management**, kilichotolewa **14th Desemba, 2018** na **Tanzania Institute of Accountancy, No. b 07766.**
2. Cheti cha **Diploma in business administration**, kilichotolewa **11th December, 2015** na **Tanzania Institute of Accountancy, No. d 13916.**
3. Cheti cha **Library Studies**, issued on **12th October, 2012** by **School of Library Archives and Documentation Studies Bagamoyo, No. 1308.**
4. Cheti cha **attendance for elementary library training** from **1st March, 2011 to 30th June, 2011** issued by school of library archives and **documentation studies Bagamoyo** and
5. **Uganda certificate of education examination 2010 no. u 2373598** at **citizen's high school, mbarara u0936/068.**

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi:DAR/KIL/RB/457841/2021**

116471402

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 122 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AMINA HAIMA DAIY OF DODOMA CITY**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY JOHN PENFORD SENYAGWA**
**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **30th Day of September, 2021**.
**Dated at Dodoma this 21st day of September 2021**

..........................................
**RESIDENT MAGISTRATE I/C**

116471102

## TANGAZO LA KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Khalifa Twahiri Nyari** anatangaza kupotelewa na hati ya umiliki wa kiwanja **namba 330 Kitalu F** Bomangombe . Kwa yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **BNG/RB/2799/2018.**

116470502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NA 40 YA 2021**
**CALVIN E. LEMA...................MDAI**
**DHIDI YA**
**EVA B. LEMA.........................MDAIWA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya madai tajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uamuzi wa madai yaliyoombwa na mdai hapo juu. Wadaawa wote wanafahamishwa kufika tarehe 30 Mwezi wa 09 Mwaka 2021 kwa ajili ya kutajwa.

**Hati hii imetolewa leo tarehe 21 Mwezi 09 Mwaka 2021.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

116470202

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**TEDDY MINJA AUGUST**
Anatangaza kwa kupotelewa kwa kadi yake ya **BAJAJI** yenye namba za usajili **MC768CGL**
Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Rb Namba.
**DAR/KIG/RB/73091/2021**

116470402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NO 88 YA 2021**

**DICKSON EYEMBE ..............................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SOZI INTERGRITY TRADING CO.LTD**
**SARA MRISHO**
**VARENTINE VALELIAN**
**SAMSON SELEMAN**
**STEPHEN JOSEPH**
**BENJAMIN SWAI**
**VENOSA KIMARIO**
**ISSACKY E. NYANDUNGE**
**RUTH EYEMBE**
**ANDREW EYEMBE ...........................................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA VENOSA KIMARIO**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 28/09/2021 mbele ya mwenyekiti E. Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 20 mwezi september 2021

116470602

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause NO.123 Of 2021**

**In the matter of the estate of the late GAUDENSIA MBOYA RIZIKI of Ipagala North within Dodoma CITY**

**And**

**In the matter of the application for letters of administration by NORBERT MUSA NJELEKELA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 day of 10 2021.
Dated at Dodoma this 21 day of 09 2021.

RESIDENT MAGISTRATE

116470702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**KESI YA "MADAI" NA. 71 YA MWAKA 2021**

**ZENICE MBOYA.......................MDAI**

**DHIDI YA**

**WALTER PHILIP SHAYO.................MDAIWA**

**KWA: WALTER PHILIP SHAYO: POPOTE ALIPO KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 23/09/2021 saa 07:00 mchana. Mbele ya Mheshimiwa Y.R. RUBOROGA - PRM.
**ANGALIA:**
Kama hukudhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 01/09/2021.**

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU -DAR ES SALAAM

116471502

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

116460202

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Sudan nusura kupinduliwa

**Juba,** SUDAN

JARIBIO la mapinduzi ya serikali ya Sudan, limetibuliwa mapema jana, kituo cha habari cha taifa nchini humo kimeripoti, kikitoa wito kwa raia kuwa na utulivu.

Wahusika katika jaribio hilo la mapinduzi hawajatajwa, serikali ikisema inadhibiti hali ya mambo.

Kwa mujibu wa vyanzo vya habari, waliohusika katika jaribio hilo la mapinduzi walitaka kudhibiti kituo cha redio ya taifa ila hawakufaulu.

**Kulikuwa na jaribio la mapinduzi lililoshindwa, lazima watu wakabiliane nalo.**

"Kulikuwa na jaribio la mapinduzi lililoshindwa, lazima watu wakabiliane nalo," vyombo vya habari vya serikali viliripoti.

Chanzo cha serikali pia kilithibitisha kwa shirika la habari la AFP kwamba wale waliopanga njama walijaribu kudhibiti jengo la shirika la utangazaji la serikali, lakini hawakufaulu.

Msemaji wa serikali alisema wanaendelea kuwahoji wanaoshukiwa kuhusika na jaribio hilo la mapinduzi litaanza muda mfupi ujao, kulingana na shirika la habari la Reuters.

Sudan inatawaliwa chini ya mkataba dhaifu wa kugawana madaraka kati ya wanajeshi na raia kufuatia kupinduliwa kwa rais wa zamani Omar al-Bashir, mwaka Aprili 2019. **RFI**



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, akizungumza juzi na wanahabari (hawapo pichani) baada ya kufanya mkutano kuhusu mabadiliko ya tabianchi, na kuzitaka nchi wanachama kutoa kiasi cha Dola bilioni 100 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kukabili mabadiliko hayo kwa nchi zinazoendelea. **PICHA; XINHUA**

## Ubelgiji, Marekani wapinga hukumu ya Rusesabagina

**Kigali,** RWANDA

UBELGIJI na Marekani zimepinga hukumu ya kifungo cha miaka 25 jela iliyotolewa na mahakama ya Rwanda dhidi ya Paul Rusesabagina zikisema, hakupewa haki ya kisheria, huku Rwanda ikiyataja madai hayo ya Ubelgiji kama dharau na kuamua kusitisha mkutano uliotarajiwa kuzikutanisha pande mbili.

Rusesabagina (pichani chini) ambaye ni mzaliwa wa Rwanda, mwenye umri wa miaka 67, ana uraia wa Ubelgiji na ana kibali cha nchini Marekani

Katika tangazo aliolitoa juzi, Naibu Waziri Mkuu wa Ubelgiji ambaye pia ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Nchi Sophie Wilmès alisema alipata taarifa kuwa hukumu ya Rusesabagina imetolewa mjini Kigali.

"Kuanzia mwanzo wa kesi hii na japokuwa Ubelgiji imekuwa ikiendelea kuomba masuala kadhaa yafanyike, inaonyesha kuwa kesi ya Rusesabagina haikuendeshwa mahakamani kwa njia iliyo ya uwazi na haki kisheria, hususan kuhusu haki yake ya kujitetea".

Wilmès alisema, serikali ya Rwanda ilisema kuwa mkutano wa kando, ambao ulitakiwa kuzikutanisha pande mbili wakati wa mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa mjini New York hautafanyika.

Baada ya kupatikana na hatia ya kushiriki katika vitendo vya ugaidi, aliyekuwa shujaa wa filamu ya Hotel Rwanda Paul Rusesabagina, hatimaye amehukumiwa kifungo cha miaka 25 jela.

Mahakama ya Rwanda ilimpata na hatia kuhusiana na mashtaka yanayohusiana na ugaidi.

Alisusia uamuzi wa kesi hiyo na hakutoka jela ili kuhudhuria mahakama. Rusesabagina alituhumiwa kwa kuwa mwanzilishi na mfadhili wa kundi moja la waasi ambalo lilitekeleza mashambulio nchini Rwanda 2018 na kuwaua watu tisa.

Mkosoaji huyo wa Rais Paul Kagame alikiri kutuma fedha kwa kundi hilo, akakana kuhusika katika mashambulizi.

Mwanawe wa kike Anaise Kanimba aliambia BBC kwamba familia yake haijaamua iwapo itakata rufaa dhidi ya uamuzi huo. **BBC**



## Ethiopia yaiondoa Tigray duru ya pili ya uchaguzi

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

ETHIOPIA imesema haitoendesha duru ya pili ya uchaguzi katika majimbo takribani 26 katika duru ijayo ya mchakato huo ya kitaifa, kutokana na masuala ya kiusalama.

Katika duru ya kwanza ya mwezi Juni, Chama cha Waziri Mkuu Abiy Ahmed, Prosperity Party, kiliweza kushinda muhula wa miaka mitano kwa kudai kushinda viti vya ubunge 410 kati ya viti 436 vya bunge la shirikisho.

Vikwazo vya usambazaji wa vifaa na ukosefu wa usalama vilisababisha ucheleweshaji wa kufanyika kwa zoezi hilo katika maeneo mengine, kwa hivyo duru ya pili ya uchaguzi imepangwa kufanyika Septemba 30.

Msemaji wa Bodi ya Uchaguzi Solyana Shimeles alisema katika uchaguzi wa sasa, zaidi ya wapigakura milioni saba watawachagua wawakilishi 47 wa bunge la shirikisho, na viti vingine 105 vya uwakilishi wa majimbo.

Hata hivyo aliongeza kusema fursa hiyo haitapatikana kwa majimbo 18 ya eneo la Amhara na manane ya Oromia.

"Bado hatujaamua kwa jinsi gani na lini uchaguzi utafanyika katika maeneo haya. Hata hivyo, kwa vile idadi ya majimbo ni ndogo, tutaamua lini tutafanya uchaguzi kwa pamoja katika maeneo yote hayo," alisema Solyana.

Eneo la Amhara limekuwa na madoa ya mapigano kati ya majeshi ya serikali na kundi la wapiganaji wa chama cha ukombozi wa watu wa Tigray, TPLF, wakati Oromia inapambana na uasi wa Jeshi la Ukombozi la Oromo OLA.

Uchaguzi huo pia hautafanyika katika baadhi ya majimbo ya kama ya Afar na Benishangul-Gumuz, bodi hiyo ilisema, ingawa haikutoa ufafanuzi wa idadi ya maeneo lengwa.

Kwa ujumla Ethiopia ina majimbo 547, bodi ya uchaguzi haikurodhesha Tigray, ambayo kwa sehemu kubwa kwa sasa ipo katika udhibiti wa TPLF. **DW**

## Kesi ya rushwa ya Zuma yaendelea

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

KESI ya rais wa zamani wa Afrika Kusini Jacob Zuma imeendelea jana, baada ya kuahirishwa mara kadhaa kwa sababu zisizojulikana.

Hivi karibuni Mahakama ya Katiba ya Afrika Kusini, ilifutilia mbali ombi la rais wa zamani Jacob Zuma akitaka ibadilishe uamuzi wake wa kumhukumu kifungo cha miezi 15 gerezani kwa kudharau mahakama.

Jacob Zuma, aliachiliwa kwa dhamana kwa sababu za afya ambazo hazikuelezwa.

Zuma, 79, amekuwa akitumikia kifungo cha miezi 15 jela kwa kudharau mahakama, tangu Julai, kufuatia kukataa kwake kufika mbele ya tume inayochunguza ufisadi chini ya utawala wake.

Alikaa mwezi mmoja tu katika gereza la Estcourt, Mashariki mwa nchi, kabla ya kulazwa hospitalini mapema mwezi Agosti na hatimaye kuachiliwa kwa dhamana. **RFI**

# SIMBA YAPEWA MBINU KUIUA MAPEMA JWANENG GALAXY

**Na Saada Akida**

WAKATI Klabu ya Simba ikijiandaa kukabiliana na Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, nahodha wa timu ya Township Rollers, Maano Ditshupo, ambao ni wapinzani wakubwa kwenye Ligi Kuu ya nchini humo, amewataka 'Wekundu wa Msimbazi' kuwa makini na kiungo mkabaji wa kikosi hicho, Gape Mohutsiwa.

Akizungumza na Nipashe jana moja kwa moja kutoka Botswana, kuhusu ubora wa wapinzani hao wa Simba, Ditshupo alisema, Jwaneng Galaxy ni moja ya timu nzuri, lakini kama mabingwa hao wa Tanzania watafanikiwa kumkamata vizuri Mohutsiwa, wanaweza kumaliza mchezo huo mapema.

"Jwaneng ni moja ya timu nzuri licha ya kwamba imeondokewa na baadhi ya wachezaji wake muhimu, lakini bado wapo vizuri, wana kiungo mkabaji mata-ta sana, anaitwa Gape Mohutsiwa.

**"Huyo ndiye kama ameibeba timu mabegani mwake, ndiye anayeanzisha mashambulizi yote, lakini ni mzuiaji mzuri wa hatari zinazoweza kuleta matatizo kwenye kikosi chake," alisema.**

Alisema klabu hiyo inao baadhi ya wachezaji wanaocheza timu ya taifa huku ikiwa na kocha mpya anayependa soka la kushambulia muda wote, hivyo lazima Simba wajipange vizuri.

Simba watacheza dhidi ya Jwaneng Galaxy kati ya Oktoba 15-17, wakianzia ugenini kabla ya kuwakaribisha Watswana hao Uwanja Benjamin Mkapa kati ya Oktoka 22-24, mwaka huu na timu itakayopata ushindi wa jumla itatinga moja kwa moja hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wekundu wa Msimbazi hao, ni kati ya timu 10 ambazo hazikuanzia hatua ya awali na badala yake zitaanzia raundi ya kwanza ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Jwaneng imetinga hatua hiyo baada ya kuitoa DFC 8ème Arrondissement ya Afrika ya Kati kwa jumla ya mabao 2-1.



Wafanyakazi wa SGA Security, wakiwa pamoja wakati wa mbio za majaribio za NMB Marathon 2021 kwenye viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. SGA ni miongoni mwa wadhamini wa mbio hizo zenye lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya kutibu wanawake wenye fistula katika Hospitali ya CCBRT. **NA MPIGAPICHA WETU**

# SGA kuendelea kudhamini michezo nchini

**Na Mwandishi Wetu**

SGA Security ambayo ni moja ya kampuni za ulinzi zinazoongoza Tanzania, imetangaza kuendelea kudhamnini michezo nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Security, Eric Sambu, alisema kampuni hiyo kwa sasa ni miongoni mwa wadhamini wa NMB Marathon 2021, mbio zitakazofanyika Jumamosi wiki hii katika viwanja vya Leaders Club, Dar es Salaam zikiwa na lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya matibabu ya wanawake wenye fistula ili kupata matibabu katika Hospitali ya CCBRT.

"SGA inaamini michezo ni muhimu kwa jamii yenye afya bora ambayo ni chachu kubwa ya maendeleo ya taifa," alisema.

Alisema udhamini huo ni sehemu ya mkakati wa SGA kuchangia katika huduma za kijamii huku ikitenga asilimia moja ya mauzo kwa huduma za kijamii kama hizo.

Katika hatua nyingine, Sambu alisema pia SGA imedhamini Tamasha la Michezo la Wanawake la Tanzanite (Tanzanite Women Sports Festival 2021), lililofanyika mwishoni mwa wiki Uwanja wa Benjamin Mkaba, Dar es Salaam na kuwakusanya zaidi ya wanamichezo 5,000 wa kike.

Tamasha hilo liliandaliwa na Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo kama ilivyoelekezwa na Rais Samia Suluhu, huku SGA ikitoa ulinzi na huduma ya kwanza na zimamoto.

Sambu alisema mwezi ujao kampuni hiyo pia itadhamini mbio za NBC Capital City hii ikiwa ni mara ya pili mfululizo.

Aidha, alisema kampuni hiyo imedhamini safari maalumu ya baiskeli ijulikanayo kama 'The Great African Cycling Safari' itakayoshirikisha nchi tano za Afrika Mashariki ambayo ilianzia Dar es Salaam Agosti Mosi, mwaka huu na kuingia nchini Kenya kupitia Tanga kisha kuelekea Mombasa, Nairobi, Kampala, Kigali, Bujumbura, Dodoma na hatimaye kumalizikia Arusha yalipo Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa upande wa soka, Sambu alisema wamekuwa wakisaidia akademi mbalimbali za ndani kukuza vipaji kwa kuwapa vifaa vya michezo na kuwafundisha masuala ya kiusalama na afya.

## Mkataba Yanga, Maliasili pale pale

**Na Adam Fungamwango**

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imesema mkataba ulioingiwa kati ya Bodi ya Utalii na Klabu ya Yanga, bado unaendelea licha ya kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumapili iliyopita.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akizungumzia suala hilo jana, alisema pamoja na kuondolewa kwenye michuano hiyo, mkataba huo bado utaendelea, na wachezaji wa Yanga wataendelea kuvaa beji yenye nembo ya maneno 'Visit Kilimanjaro & Zanzibar' kwa kuwa bado wataendelea kuonekana kwenye televisheni watakapokuwa wakicheza mechi zao popote pale hapa nchini.

"Kwanza niwapongeze Yanga kwa kuwa wazalendo kwa sababu wamejitolea bure kutangaza vivutio vilivyopo nchini na kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele kutangaza utalii.

"Ni kweli Yanga imetolewa, lakini mkataba ule haukuwa kwa mechi za nje ya nchi tu, wataendelea kuonyesha vivutio vyetu hata kwenye mechi za ndani. Yanga ni timu kubwa yenye mashabiki wengi ndani na nje ya nchi ambao wanafuatiliwa kwenye mitandao ya kijamii na televisheni," alisema Waziri huyo.

## Ruvu Shooting yaja na usiku wao Sept. 25

**Na Donald Lukele,** TUDARCo

TIMU ya Ruvu Shooting imetangaza rasmi ujio wa siku ya kutambulisha kikosi chao cha msimu mpya waliyoibatiza kwa jina la "Usiku wa Ruvu Shooting" itakayofanyika Septemba 25, mwaka huu, Mlandizi mkoani Pwani.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Masau Bwire, alisema katika kampeni yao yakuhakikisha wanachukua ubingwa au kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa, wameamua kuja tofauti na misimu yote kwa kusajili kikosi bora na kukitambulisha rasmi katika tamasha hilo maalum.

"Kikosi chetu ni bora kuliko msimu uliopita na tumesajili wachezaji wapya takriban 11, tutakitambulisha siku hiyo na kitacheza mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya Mlandizi Combine," alisema Bwire huku akiongeza kuwa mgeni rasmi wa Usiku wa Ruvu Shooting atakuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge.

## ZISIKUPITE

### KASSIE KUMRITHI POGBA

KLABU ya Manchester United wamemtambua kiungo wa AC Milan na Ivory Coast, Franck Kessie, 24, kama mbadala wa nyota wa Ufaransa, Paul Pogba, 28, ambaye mkataba wake Old Trafford unamalizika mwaka 2022. ***(Mundo Deportivo)***

### NDOMBELE KWENYE RADA

MCHEZAJI mwenzake na Paul Pogba katika Timu ya Taifa ya Ufaransa, Tanguy Ndombele, ni kiungo mwingine ambaye yupo kwenye rada za Manchester United, ambaye alihamia Tottenham Hotspur kwa pauni milioni 53.8 mwaka 2019. ***(Calciomercato)***

### CHRISTENSEN, MKATABA MPYA

MLINZI wa Denmark, Andreas Christensen yuko tayari kusaini nyongeza ya mkataba huko Chelsea yenye thamani ya pauni 120,000 kwa wiki baada ya awali kupewa ofa ya mshahara wa chini zaidi, pauni 78,000. ***(Sun)***

### SAKA AWANIWA ULAYA

JUVENTUS na Atletico Madrid ni miongoni mwa klabu zinazomwangalia winga wa Arsenal na England, Bukayo Saka, 20. ***(Calciomercato)***

### DRINKWATER AKIRI UGUMU

KIUNGO wa England, Danny Drinkwater, 28, anakiri maisha yake ya Chelsea yamekuwa 'katika hali mbaya baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuanza kucheza Reading katika uhamisho wa mkopo wake wa nne mbali na Stamford Bridge. ***(talkSPORT)***

### SANCHEZ KUACHANA NA INTER

KLABU ya Inter Milan ina hamu ya kumwachia mshambuliaji wake, Alexis Sanchez, 32, huku Real Betis na Sevilla wakionyesha nia ya kumsajili. ***(InterLive)***

### MARQUINHOS ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid inapanga kumsajili beki wa Paris St-Germain, Marquinhos, 27, mwenye huku Mbrazil huyo akiwa chini ya mkataba katika klabu hiyo ya Ufaransa hadi mwaka 2024. ***(Fichajes)***

### JUVE YAMPOTEZEA POGBA

WAKATI hatima ya Paul Pogba kule Manchester United bado haijulikani, Juventus haipangi kumrudisha Mfaransa huyo Turin. Pogba alishinda mataji manne ya Serie A katika misimu yake pale Juve kabla ya kurudi Old Trafford mwaka 2016. ***(Tuttomercatoweb)***

### LEEDS YAMTAKA NOA

KLABU ya Leeds United bado inavutiwa na winga wa Uholanzi na Club Bruges, Noa Lang, 22. ***(Football Insider)***

### DUSAN KUFUNGWA FIORENTINA

KLABU ya Fiorentina inajaribu kumfunga mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic, 28, kwa mkataba mpya baada ya mchezaji huyo kuhusishwa na kuhamia Tottenham Hotspur msimu ujao wa majira ya joto. ***(Gazzetta dello Sport via Sport Witness)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL AIONA INJINI YA KANTE KIKOSI CHELSEA

**N'Golo ni mchezaji bora, ukiwa naye, una kitu kila mtu anakitafuta, ni mtu wa kipekee...**

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amemtaja kiungo N'Golo Kante kama mchezaji aliyeleta mabadiliko katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tottenham, Jumapili.

Kante alitokea benchi kuchukua nafasi ya Mason Mount katika kipindi cha pili cha dabi hiyo ya London na kuwasaidia 'Blues' hao kuibuka na alama zote tatu muhimu.

**Kante aliifungia timu yake bao la pili la mchezo na kumvutia kocha huyo raia wa Ujerumani na uchezaji wake katika mchezo huo.**

"Alicheza kwa sehemu kubwa. N'Golo ni N'Golo, ni wa kipekee, wa aina yake na kuwa naye uwanjani hufanya tofauti kubwa kwa kila kitu," alisema Tuchel akiiambia BBC Sport.

"Kuwa na Kante kwenye kikosi ni sehemu ya kufurahisha, kwa sababu anaweza kufanya chochote katika wakati wowote, kwa hakika ni mmoja wa wachezaji muhimu sana kwenye kikosi changu."

Aliongeza: "(N'Golo) ni mchezaji bora. Ukiwa na N'Golo, una kitu kila mtu anatafuta.

MECHI KALI
HOME
MANCHESTER UTD
1.55 | 4.00 | 5.58
WEST HAM
AWAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 517,

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888,
KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN UNITED KUWAUZA VAN DE BEEK, MARTIAL



**MANCHESTER,** England


KLABU ya Manchester United imetangaza kwamba, inampango wa kuwauza wachezaji wake saba katika dirisha dogo la usajili la Januari.

Kwa mujibu wa The Sun, Man United imewaweka sokoni wachezaji Donny van de Beek, Jesse Lingard, Phil Jones, Eric Bailly, Anthony Martial, Diogo Dalot na Alex Telles.

Lingard ni moja ya wachezaji ambao wapo kwenye mipango ya kuuzwa ingawa Kocha Ole Gunnar Solskjaer alisema kwamba, mchezaji huyo yupo katika mipango yake msimu huu.

'Mashetani Wekundu' hao wameamua kufanya, hivyo kwa kile wanachodai kwamba wanapunguza gharama za matumizi klabuni hapo.

Vilevile Man United wana mpango wa kuwatoa kwa mkopo wachezaji wa timu ya vijana, ili wakapate uzoefu katika kikosi cha kwanza.



# Mshahara wa Messi PSG wawekwa wazi

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi alijiunga na klabu ya Paris Saint-Germain wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto kama mchezaji huru, lakini mshahara wa mchezaji huyo wa Argentina haukuwekwa wazi na sasa klabu hiyo ya Ufaransa imebainisha.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, zinadai kwamba Messi atalipwa euro milioni 30 kwa misimu miwili ijayo na kiasi hiki kinaweza kufikia hadi euro milioni 40 kama akiongeza mwaka mmoja pale Paris.

Kiasi hicho hakihusiani na mapato binafsi ambayo mchezaji anaweza kupata na bonasi za timu wakati wa msimu.

Kingine ni kwamba Messi atakuwa akitengeneza kiasi cha euro milioni moja kupitia tokeni ya mashabiki ya PSG ya fedha ya matandaoni. Klabu ya PSG ilisaini dili na Crypto.com na itapata faida kati ya milioni 25 hadi 30 kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Michezo wa Klabu hiyo, Leonardo amebainisha kwamba, kinachosemwa kuhusu mshahara wa Messi hakina ukweli wowote.

"Najua kwamba watu wanazungumza sana, lakini ukweli uko tofauti kabisa na kile kinachosemwa," alisema akinukuliwa na Jarida la France Football.

HABARI MICHEZO

# BARCA YAFUNGUKA OFA YA FATI UNITED



**MANCHESTER,** England

BARCELONA imeripotiwa kuwa ilikataa ofa ya pauni milioni 85 kutoka Manchester United kwa ajili ya uhamisho wa Ansu Fati katika dirisha la uhamisho la msimu wa majira ya joto wa 2020.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alishiriki kampeni ya ligi ya msimu wa 2019-20 na kufanya vema, akifunga mabao saba katika mechi 24 za LaLiga.

Fati alifunga mabao matano na kutoa asisti nne kwenye mechi 10 katika mashindano yote mwaka jana kabla ya kupata jeraha kubwa la goti ambalo limemweka nje ya uwanja kwa miezi 10 iliyopita.

Kiwango cha nyota huyo katika msimu wa 2019-20, kiliwavutia Man United na kuamua kutoa ofa.

Kwa mujibu wa AS, 'Mashetani Wekundu' hao waliwasilisha ofa ya pauni milioni 85 kwa ajili ya huduma ya nyota huyo, wakati huo walikuwa wakijaribu kumsajili Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund.

Barcelona inasemekana ilikataa moja kwa moja ofa hiyo, na kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer badala yake kikawekeza dau la pauni milioni 73 kwa Sancho katika msimu wa majira ya joto wa 2021.




# FIFA kujadili Kombe la Dunia miaka miwili

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (FIFA), limeyaalika mashirikisho yote duniani kwenye mkutano mwisho wa mwezi huu kujadili kalenda ya kimataifa, pamoja na pendekezo la Arsene Wenger la Kombe la Dunia kufanyika kila baada ya miaka miwili.

FA na SFA wamealikwa kwenye mkutano huo utakaofanyika Septemba 30, mwaka huu, pamoja na vyama vingine vyote wanachama wa shirikisho la mpira wa miguu duniani.

Mkutano wa kwanza wa mtandaoni ni pamoja na mialiko tofauti iliyotumwa na FIFA mapema mwezi huu kwa wadau wa soka wakiwamo mashirikisho yote, Jumuiya ya Klabu za Ulaya, Jukwaa la Ligi duniani na Umoja wa Wachezaji duniani, FIFPRO.

Mada kuu ya majadiliano inapaswa kuwa pendekezo la kubadilisha kalenda ya kimataifa kwa kufanya Kombe la Dunia kila baada ya miaka miwili, mpango ulioongozwa na kocha wa zamani wa Arsenal, Wenger, ambaye sasa ni mkuu wa maendeleo ya soka duniani wa FIFA.

"Kuna makubaliano mapana ndani ya mchezo kwamba kalenda ya mechi za kimataifa inapaswa kurekebishwa na kuboreshwa," ilisema taarifa iliyotolewa na FIFA Jumatatu.

350,800

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/09/21 | 17:00 | Leeds vs West Ham | 2.71 | 3.57 | 2.46 |
| 02. 25/09/21 | 17:00 | Watford vs Newcastle | 2.37 | 3.32 | 3.01 |
| 03. 25/09/21 | 17:00 | Blackpool vs Barnsley | 2.52 | 3.31 | 2.66 |
| 04. 25/09/21 | 17:00 | Swansea vs Huddersfield | 2.27 | 3.26 | 3.06 |
| 05. 25/09/21 | 17:00 | Nottingham vs Millwall | 2.81 | 3.05 | 2.56 |
| 06. 25/09/21 | 17:00 | Blackburn vs Cardiff | 2.34 | 3.24 | 2.95 |
| 07. 25/09/21 | 17:15 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.21 | 2.91 |
| 08. 25/09/21 | 18:00 | St Etienne vs Nice | 2.94 | 3.24 | 2.40 |
| 09. 26/09/21 | 15:00 | Mallorca vs Osasuna | 2.91 | 3.06 | 2.61 |
| 10. 26/09/21 | 16:00 | Southampton vs Wolverhampton | 2.57 | 3.22 | 2.82 |
| 11. 26/09/21 | 16:00 | Udinese vs Fiorentina | 2.66 | 3.31 | 2.66 |
| 12. 26/09/21 | 18:30 | Arsenal vs Tottenham | 2.41 | 3.17 | 3.07 |
| 13. 26/09/21 | 19:00 | Lazio vs Roma | 2.75 | 3.65 | 2.39 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 22 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4681 | FC Tokyo vs Nagoya Grampus | 2.37 | 3.00 | 2.95 |
| 13:30 | 1682 | Brisbane Knights vs THE Gap | 1.61 | 4.25 | 4.16 |
| 16:30 | 1011 | Loko Vltavin vs Banik Ostrava | 12.54 | 7.33 | 1.14 |
| 17:00 | 5805 | SK Lisen vs Sparta Prague | 10.60 | 6.36 | 1.19 |
| 17:15 | 2875 | Slovan Velvary vs Slavia Prague | 25.29 | 11.67 | 1.03 |
| 17:30 | 4420 | Kjellerup IF vs Midtjylland | 38.91 | 19.45 | 1.01 |
| 18:30 | 5825 | Inter Turku vs AC Oulu | 1.43 | 4.24 | 6.36 |
| 19:00 | 1893 | Nykobing FC vs Copenhagen | 11.61 | 6.77 | 1.16 |
| 19:00 | 3405 | Lausanne-Sport vs BSC Young Boys | 5.51 | 4.53 | 1.49 |
| 19:00 | 4140 | Fremad Amager vs Randers | 4.65 | 3.78 | 1.63 |
| 19:00 | 4876 | Ruzomberok vs Slovan Bratislava | 5.82 | 3.88 | 1.50 |
| 19:30 | 2469 | Salernitana vs Verona | 3.58 | 3.38 | 2.09 |
| 19:30 | 5947 | Spezia vs Juventus | 7.07 | 4.84 | 1.41 |
| 19:45 | 2009 | NEC Nijmegen vs Utrecht | 4.44 | 3.80 | 1.71 |
| 19:45 | 2340 | GO Ahead Eagles vs PSV Eindhoven | 9.50 | 5.74 | 1.26 |
| 20:00 | 1129 | Rennes vs Clermont Foot | 1.98 | 3.48 | 3.68 |
| 20:00 | 2036 | Sirius FK vs Norrkoping | 2.85 | 3.43 | 2.21 |
| 20:00 | 2392 | Montpellier vs Bordeaux | 1.97 | 3.64 | 3.54 |
| 20:00 | 2440 | Elfsborg vs Malmo | 3.04 | 3.43 | 2.11 |
| 20:00 | 2634 | Kayserispor vs Galatasaray | 4.53 | 3.65 | 1.72 |
| 20:00 | 2730 | Lille vs Reims | 1.67 | 3.66 | 5.15 |
| 20:00 | 3040 | Monaco vs St Etienne | 1.52 | 4.19 | 5.99 |
| 20:00 | 5108 | Nantes vs Brest | 2.10 | 3.33 | 3.48 |
| 20:00 | 5668 | Goeztepe vs Hatayspor | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 20:00 | 5914 | Djurgardens IF vs Degerfors | 1.23 | 5.64 | 9.33 |
| 20:00 | 5927 | Orebro SK vs Ostersunds | 1.97 | 3.34 | 3.49 |
| 20:30 | 2860 | Espanyol vs Alaves | 1.82 | 3.40 | 4.71 |
| 20:30 | 5650 | Sevilla FC vs Valencia | 1.67 | 3.77 | 5.23 |
| 21:00 | 1812 | Groningen vs Vitesse Arnhem | 2.46 | 3.41 | 2.67 |
| 21:00 | 2203 | Shakhtar Donetsk vs Dynamo Kiev | 2.51 | 3.28 | 2.56 |
| 21:30 | 1371 | Brighton vs Swansea | 1.43 | 4.24 | 7.11 |
| 21:30 | 4219 | St. Gallen vs FC Basel | 2.90 | 3.59 | 2.21 |
| 21:30 | 4997 | CS Hunedoara vs Steaua Bucuresti | 11.66 | 6.61 | 1.17 |
| 21:45 | 1023 | Chelsea vs Aston Villa | 1.44 | 4.43 | 6.50 |
| 21:45 | 1307 | Millwall vs Leicester | 4.15 | 3.60 | 1.80 |
| 21:45 | 1582 | Royal Antwerp vs Racing Genk | 3.01 | 3.75 | 2.10 |
| 21:45 | 2708 | Manchester Utd vs West Ham | 1.55 | 4.00 | 5.58 |
| 21:45 | 3971 | AC Milan vs Venezia | 1.26 | 6.24 | 10.06 |
| 21:45 | 4035 | Cagliari vs Empoli | 2.00 | 3.71 | 3.51 |
| 21:45 | 4263 | Arsenal vs AFC Wimbledon | 1.14 | 7.21 | 17.60 |
| 21:45 | 4606 | Wolverhampton vs Tottenham | 2.35 | 3.21 | 2.96 |
| 22:00 | 2187 | Metz vs Paris St Germain | 8.55 | 5.46 | 1.31 |
| 22:00 | 2732 | PEC Zwolle vs Sparta Rotterdam | 2.68 | 3.27 | 2.53 |
| 22:00 | 3283 | Feyenoord vs Heerenveen | 1.38 | 4.94 | 6.71 |
| 22:00 | 3993 | Lyon vs Troyes | 1.40 | 4.98 | 6.57 |
| 22:00 | 4217 | Lens vs Strasbourg | 1.97 | 3.54 | 3.64 |
| 22:00 | 5295 | Lorient vs Nice | 3.14 | 3.38 | 2.22 |
| 22:00 | 5395 | Angers vs Marseille | 3.43 | 3.38 | 2.10 |
| 23:00 | 1308 | Villarreal vs Elche | 1.51 | 4.11 | 6.62 |
| 23:00 | 5788 | Real Madrid vs Mallorca | 1.29 | 5.47 | 10.04 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Septemba 22, 2021
Nipashe



Tuchel aiona injini ya Kante Chelsea UKURASA 21

UDHAMINI...



Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez (kushoto), akibadilishana mkataba na Mkurugenzi wa Kampuni ya Emirates Aluminium, Doe Marandu, baada ya kampuni hiyo kuingia makubaliano ya udhamini wa miaka miwili na timu hiyo wenye thamani ya Sh. milioni 300 kwa ajili ya zawadi kwa mchezaji bora wa kila mwezi katika msimu wa Ligi Kuu Bara 2021/22. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kesi Morisson, Yanga mtifuano mkali FIFA

**Na Tunu Hassan,** TUDARCo

KESI ya aliyekuwa winga wa Yanga, Bernard Morrison na klabu hiyo iliyokuwa ikitarajiwa kutolewa hukumu yake Ijumaa wiki hii, mtifuano wa pande hizo mbili katika Mahakama ya Usuluhishi ya Mambo ya Michezo duniani (CAS), unaelekea kuwa mkali baada ya kupigwa tena kalenda hadi Oktoba 26, mwaka huu.

Yanga ilikata rufaa CAS ikipinga hukumu ya Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania, kumtangaza Morrison kuwa ni mchezaji huru baada ya kukuta kuwapo kwa kasoro katika mkataba wake na mchezaji huyo raia wa Ghana.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, wakili anayesimamia kesi hiyo kwa upande wa Klabu ya Yanga, Alex Mgongolwa, alisema wamepokea taarifa kutoka CAS ikiwaeleza kuwa hukumu ya kesi hiyo sasa itatoka Oktoba 26, mwaka huu badala ya Septemba 24 kama ilivyokuwa hapo awali.

Mgongolwa, alisema mtoa hoja ana hoja ndiyo maana inasubiriwa kuona majibu yatakuaje mpaka sasa, na kwamba kama kungekuwa hakuna hoja suala hilo lisingeendelea mpaka leo na majibu yangeshapatikana.

"Unajua wameleta hiyo taarifa nyingine ikisema wameahirisha mpaka Oktoba 26, lakini hawakusema sababu ni nini, lakini kwa uzoefu tu wa mambo haya, siku zote ukiona shauri linachukua muda mrefu basi mleta shauri inawezekana ana hoja ndiyo maana unaona hivyo.

"Siku zote uamuzi unakuwa mwepesi pale ambapo shauri linakuwa halina mashiko, kwa hiyo tunasubiri uamuzi hayo kuona itakuaje. Sisi hatujawajibu chochote zaidi ya hiyo taarifa yao tu ambayo tumeipokea, na tupo tayari kupokea majibu yao," alisema Mgongolwa.

# Simba: Yanga haitoki, Ngao yetu

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### Wenyewe wasema tupo fiti njooni, TFF yatangaza kuziona buku 10 huku ikieleza...

WAKATI homa ya mechi ya watani wa jadi ikizidi kupanda huku Shirikisho la Soka nchini (TFF), likitangaza viingilio vya mchezo huo maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2021/22, mabingwa wa soka nchini, Simba, wamesema wapinzani wao, Yanga wasahau kutwaa Ngao ya Jamii kwa sababu kwa sasa wanaichukuliwa kama ni mali yao.

**Vigogo hivyo vya soka nchini, vitakutana Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na baada ya mchezo huo wa kuwania Ngao ya Jamii, msimu mpya wa Ligi Kuu 2021/22, utakuwa umezinduliwa rasmi ambapo utaanza Septemba 27, mwaka huu.**

Mratibu wa Klabu ya Simba, Abbas Ally, amesema kwa sasa timu yao imesharejea kambini baada ya mapumziko ya siku moja, lilipomalizika Tamasha la Simba Day na sasa ni rasmi wamefungua msimu mpya wa mashindano.

"Sisi tumeshaichukua Ngao ya Jamii mara mbili mfululizo. Ni mali yetu sasa, kwa hiyo hatuwezi kuiacha. Hatuwezi kumuachia mtu yeyote Ngao ya Jamii," alisema mratibu huyo.

Alisema wanachoshukuru ni kwamba baada ya kumalizika mechi dhidi ya TP Mazembe na kuchapwa bao 1-0 Jumapili iliyopita, hapakuwa na mchezaji yeyote majeruhi, hivyo timu inakwenda kuanza msimu ikiwa na wachezaji wote 32 iliyowasajili.

"Hii ni faraja kwetu na kocha atakuwa na chaguo pana zaidi kwani atakuwa na wachezaji wake wote, kwa sababu tuna mechi mfululizo. Tukitoka kucheza dhidi ya Yanga Jumamosi, tuna mechi nyingine Musoma na Dodoma," alisema mratibu huyo.

Akizungumzia maandalizi alisema kwa sasa kocha anarekebisha upungufu aliyouona kwenye mechi zilizopita.

"Si mechi ya TP Mazembe peke yake, hata zile mechi za kirafiki tulizocheza Morocco na Arusha nazo pia zilikuwa na makosa kadhaa ambayo yanahitaji kurekebishwa na wakati wake ni huu," alisema.

Kwa upande wa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wamerejea na wanaendelea kujiandaa vizuri kwa ajili ya kufanya vizuri kwenye mechi ya hiyo.

"Baada ya mchezo wetu dhidi ya Rivers United kule Port Harcourt, Nigeria, wachezaji wote wamehamishia mawazo yao kwenye 'derby' wikiendi hii, mechi hii ndio mwanzo wetu wa kuanza vema kwenye ligi na kutwaa mataji na kufikia malengo yetu ya kurejesha heshima ya klabu hii," alisema Bumbuli.

Alisema wachezaji wako fiti na nyota watatu ambao hawakucheza dhidi ya Rivers United, Fiston Mayele, Shaaban Djuma na Khalid Aucho watakuwapo kwenye mchezo huo.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, akitangaza viingilo vya mechi hiyo, alisema jukwaa la VIP A litakuwa ni kwa ajili ya watu maalum, huku VIP B kiingilio kikiwa ni Sh. 30,000, VIP C na viti vya rangi ya machungwa Sh. 20,000 na viti vya bluu na kijani Sh. 10,000.

Alisema wametaja viingilio hivyo mapema ili mashabiki na wadau wa soka kujiandaa na ndani ya hizi siku mbili watawaeka wazi vituo vitakavyouzwa tiketi hizo.

"Kwa upande wa TFF maandalizi yanaenda vizuri, kuelekea mchezo huo na siku mbili kabla ya mechi tutawaeleza vituo vya kununua tiketi za mechi hiyo ya ufunguzi wa ligi," alisema Ndimbo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >